# Nipashe

Alhamisi Julai 2, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580273

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Profesa Mkumbo ajitosa kuwania ubunge Ubungo

UKURASA 4

# CHADEMA yapuliza kipenga Zanzibar

**TAREHE** kumpata mgombea urais yatajwa, ratiba wawakilishi, madiwani hadharani...*Endelea ukurasa 2*





Askari Polisi akisimamia kufukua mwili wa Tulizo Konga (38), aliyezikwa siku 90 zilizopita, kwa kibali cha mahakama katika kijiji cha Igumbilo, kata ya Chimala, Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya jana, kwa ajili ya uchunguzi zaidi, baada ya ndugu kutilia shaka kifo chake. **PICHA NDOGO:** Jeneza lenye mwili baada ya kulitoa kaburini. **Habari uk. 16. PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Viongozi CCM, UWT wanaswa TAKUKURU tuhuma za rushwa

UKURASA 2

## HADHARI UPEPO MKALI NCHINI

UKURASA 2

### BAA LA CORONA



Hatari ya kupata Covid-19 sehemu ya kazi itategemea kama watu hawaachiani nafasi ya mita moja na kugusana na mtu mwenye maambukizi. WHO

- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



**MICHEZO** YANGA YATAMBA HAISHIKIKI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# CHADEMA yapuliza kipenga Zanzibar

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA), kimetoa ratiba ya utaratibu wa kupata wagombea wa urais, uwakilishi na udiwani visiwani Zanzibar huku mgombea urais visiwani humo kupitia chama hicho akitarajiwa kujulikana Julai 29.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na Ofisi ya Chama hicho Makao Makuu Zanzibar, uchukuaji wa fomu za urais, kutafuta wadhamini na kuzirejesha, utaanza rasmi Julai 4 hadi 19 saa 10 jioni.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Julai 20, Kamati Maalum itaketi kupitia majina ya wagombea wa nafasi hiyo ya urais na kuwasilisha ripoti yake mbele ya Kamati Kuu.

Pia, Julai 22, Kamati Kuu itapendekeza jina la mgombea au wagombea wa urais na 29 mwezi huo itaketi mkutano mkuu kwa ajili ya kuteua mgombea wa urais wa kupeperusha bendera ya chama hicho.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa wagombea wa nafasi za ubunge na uwakilishi utaanza Julai 4 hadi 10.

Ilielezwa zaidi katika taarifa hiyo kuwa, kura za maoni na uteuzi wa awali wa kamati za utendaji utafanyika Julai 13 hadi 17, wakati Julai 25 Kamati Maalum itafanya uteuzi wa awali wa wagombea wa ubunge na uwakilishi na Julai 30 hadi 31, Kamati Kuu itateua wagombea wa nafasi hizo.

"Julai 11 hadi 17 itakuwa ni kuchukua na kurejesha fomu za udiwani, Julai 20 hadi 23, kura za maoni zitakusanywa na Kamati ya Utendaji Kanda na Julai 24 itakuwa ni kamati za utendaji kuteua wagombea wa nafasi hizo," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Kwa upande wa ubunge na uwakilishi viti maalum, taarifa hiyo ilisema kuwa, kuanzia Julai 4 hadi 10, itakuwa ni uchukuaji na urejeshaji, Julai 13 hadi 17 itakuwa ni mahususi kwa kura za maoni na uamuzi wa kamati za utendaji.

Ilieleza kwamba Septemba 14, Kamati Maalum itapitia na kufanya uteuzi wa awali wa wagombea na kuwasilisha ripoti yake mbele ya Kamati Kuu na Julai 14 hadi 25, wagombea wateuliwa.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa ajili ya wagombea wa udiwani viti maalum, utafanyika kuanzia Julai 11 hadi 17, wakati Julai 20 hadi 23 itakuwa ni kura za maoni na kamati za utendaji.

"Kamati Maalum itafanya uteuzi wa awali wa nafasi hiyo za udiwani viti maalum na kuwasilisha ripoti yake mbele ya Kamati Kuu Septemba 14, na Julai 14 hadi 15, Kamati Kuu itateua wagombea wa nafasi hizo.



Daladala lenye namba za usajili T 489 CHM, linalofanya safari zake Kitunda Mwanagati na Mnazi Mmoja, likiwa limepinduka baada ya kushindwa kupanda mlima, eneo la Sirali, Kivule, jijini Dar es Salaam jana, huku likiwa limebeba wanafunzi wa Shule za Sekondari Kivule na Abuu Jumaah, baadhi yao walijeruhiwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viongozi CCM mbaroni kwa tuhuma za rushwa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

VIONGOZI wawili wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Shinyanga, wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa tuhuma za rushwa.

Wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo hivyo ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM, Asha Makwaiya, na Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Tawi la Mshikamano, Elizabeth Itete. Mbali na viongozi hao, pia wamo wajumbe 10 wa UWT.

Mkuu wa Takukuru mkoani Shinyanga, Hussein Mussa, alisema jana kuwa viongozi na wanachama hao walikamatwa Juni 28, mwaka huu, nyumbani kwa Itete wakipokea vitu hivyo.

Alisema baada ya kupata taarifa juu ya kutokea kwa tukio hilo, maofisa wa Takukuru walifika nyumbani kwa Itete na kumkuta Makwaiya na wajumbe hao wa UWT wakiwa na vitenge, kandambili na mashuka kwa ajili ya kutoa na kupokea rushwa.

"Tulimkamata Asha Makwaiya ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM, akiwa nyumbani kwa Elizabeth Itete ambaye ni Katibu wa UWT Tawi la Mshikamano, akitaka kutoa rushwa kwa wajumbe hao ili kushawishi achaguliwe au kuchaguliwa kwa aliyemtuma kuwa kiongozi katika uchaguzi mkuu," alisema Mussa.

Aliongeza kuwa: "Tunawashikilia pia wajumbe 10 wa UWT Kata ya Ngokolo ambao tuliwakuta nyumbani kwa katibu wa UWT wakiwa na Makwaiya, wakitaka kupokea rushwa. Bado tunaendelea na uchunguzi dhidi yao kutokana na kudai kuwa waliitwa tu hawakujua kama kuna kupewa rushwa."

Kutokana na kujitokeza kwa hali hiyo, Mussa aliwataka wananchi wa mkoa wa Shinyanga, kuendelea kutoa taarifa katika taasisi hiyo hasa katika kipindi hiki cha kuanza mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama kwa ajili ya kuwania nafasi za ubunge na udiwani.

## TMA yatahadharisha upepo mkali nchini

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa vipindi vya upepo mkali unaofika kilometa 50 kwa saa na mawimbi yatakayofikia zaidi ya mita mbili kwenye Bahari ya Hindi.

Hali hiyo inatarajiwa kutokea katika kipindi cha kuanzia Julai Mosi hadi 4.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Menaja wa Kituo Kikuu cha Utabiri cha TMA, Samwel Mbuya, maeneo yatakayoathirika na upepo huo ni mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Zanzibar, Mafia, Lindi na Mtwara.

Pia, alisema hali hiyo inatarajia kutokea katika maeneo yanayozunguka maziwa makuu ya Tanganyika na Nyasa katika mikoa ya Kigoma, Songwe, Mbeya na Ruvuma.

"Wananchi katika maeneo haya wanapaswa kuchukua tahadhari kwa sababu kutakuwa na athari ya kusimama kwa huduma za usafiri na kiuchumi," alisema Mbuya kwenye taarifa hiyo.

Mamlaka imewataka wananchi kuendelea kufuatilia taarifa ya hali ya hewa zitakazotolewa na mamlaka ili kuendelea kuchukua tahadhari.

"Mamlaka inaendelea kufuatilia kwa karibu mifumo ya hali ya hewa na tutakuwa tukitoa taarifa kwa wananchi kila wakati, lakini ni vyema pia kuanza kuchukua tahadhari mapema kila taarifa inapotolewa," alisema Mbuya.

Alisema hali inatarajiwa kutulia kuanzia Julai 5, katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi.

## Zitto, Bwege watinga polisi

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, na viongozi wengine saba wameripoti kituo kikuu cha polisi Lindi kama walivyotakiwa na Jeshi la Polisi.

Kiongozi huyo na mbunge wa Kilwa Kusini, Suleiman Bungara, maarufu kama Bwege, pamoja na wengine, walikamatwa Juni 23, mwaka huu, kwa madai ya kuhatarisha amani.

Jana, baada ya kuripoti walitakiwa kurudi tena Julai 20, mwaka huu, huku chama hicho kikilalamikia usumbufu kwa kiongozi wao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Naibu Katibu wa Kamati ya Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma, Janeth Rithe, chama hicho kitaendelea na shughuli zake za kisiasa bila kujali usumbufu.

"Licha ya vitisho vya mara kwa mara kutoka kwa jeshi la polisi, jana Kabwe amerejea Kilwa kuwapokea madiwani na kufanya kikao na viongozi na wanachama wa ACT," alisema.

Alisema ziara hizo ni endelevu katika maeneo mbalimbali nchini na kuwaomba wanachama wao kuendelea kuwaunga mkono.



## TANGAZO

# MIAKA 25

## YA KUJENGA MAFANIKIO YA KIFEDHA KWA NCHI YETU NA WATEJA WETU



**Kwa wateja wetu, wadau na marafiki zetu,**

Robo karne iliyopita Benki ya Stanbic iliingia nchini Tanzania baada ya kuinunua benki ya Meridian. Tunapoadhimisha hatua hii muhimu, tunatambua kuwa mafanikio yetu yametokana na mchango kutoka wadau wetu muhimu; taifa; wateja wetu; wafanyakazi na jamii nzima kwa ujumla. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wote waliotuunga mkono katika safari hii.

Milango ya tawi letu la kwanza ilifunguliwa mnamo mwaka 1995 ndani ya jiji la Dar es Salaam ambalo linatambulika kama kitovu cha fursa na ndoto. Na wakati huo, taifa la Tanzania lilikuwa limepitia kipindi cha kuwa na uchumi huria, jambo lililohusisha upanuzi wa shughuli mbalimbali za kifedha pamoja na ukuaji maradufu wa pato la taifa. Sisi kama benki ya Stanbic tunafurahi kuwa sehemu ya wachangiaji wa utajiri wa historia hii. Na pia tunaazimia kuendelea kukua kwa kupanua wigo wetu, bidhaa zetu, huduma zetu, ambazo zinatuwezesha kufikia mategemeo ya wateja na wadau wetu.

katika kipindi cha miaka 25 tumefanikiwa kutoa huduma za kibenki kwa kiwango cha daraja la kwanza kwa wateja wetu wa aina mbalimbali; watu binafsi, biashara ndogo na kati; pamoja na makampuni makubwa ya kitaifa na kimataifa. Yote haya ni kwa ajili ya kuunda ngome madhubuti za kibiashra na kutimiza njozi ndani ya taifa letu.

Hakika tunaona fahari kusema upekee unaoletwa na maadhimisho haya ni pamoja na kumbukumbu kwamba tumejenga ngome imara, lakini zaidi ni uwajibikaji wetu katika kulichangia taifa hili ambalo tunalitambua kama nyumbani kwetu.

Tukipitia mafanikio yetu, tunaona kwamba tumefanikiwa kuleta huduma zenye mapinduzi makubwa sokoni, mfano huduma "Bulk payment solution" kwa kutumia simu ya mkononi imeboresha ufanisi na usalama katika utendaji wa shughuli za kibiashara. Mfano mwingine wa kipekee ni uwepo wa mashine za ATM zenye uwezo wa kuweka fedha – jambo linalotupa uwezo wa kuhudumia wateja wetu kwa saa 24. Vile vile, tumetambulisha mashine iitwayo, 'Cash Deposit Machine' ambayo imewawezesha wateja wetu wa kibiashara kuweka fedha nyingi kwa wakati mmoja na haraka. Pia tunaendelea kupanua wigo wetu, kwani hivi karibu tumezindua tawi jipya mkoani Dodoma.

Tukiwa kama shirika lenye mizizi yake ndani ya bara la Afrika kwa takribani miaka 155, katika mataifa ya kiafrika 20 na vituo 5 vya kifedha duniani kote, tunaamini kwamba tunauwezo wa kuendelea kuichochea Tanzania kuweza kufikia malengo yake. Tunafanya jambo hili kwa kuchangia miradi mbalimbali ya miundombinu kama vile, umeme, maji, barabara, viwanja vya ndege, elimu, mawasiliano na nishati – ili kuhakikisha tunachangia kuboresha maisha ya kila mtanzania.

Uwezo wetu wa kuitikia wito wa msaada wa haraka kwa wateja wetu wanapopitia changamoto – kama vile kuanzishwa kwa 'Africa China Agency Proposition' yenye kuhakikisha kuwa wateja wetu wanaendelea kufanya biashara ilhali wakikabiliana na janga la COVID-19, ni ushuhuda tosha wa azma tuliyonayo katika kuchochea ukuaji wa bara la Afrika. Wateja pia wanafursa ya kutazamia huduma nyingine bora zaidi katika siku zijazo mwaka huu mfano; Huduma ya kufungua akaunti ya benki kwa simu ya mkononi, huduma ya mikopo ya papo kwa papo kiganjani na huduma ya benki kupitia mawakala.

Ushirikiano wenu umetuwezesha kutambuliwa katika tuzo mbalimbali kama vile Benki bora ya mwaka, Benki bora ya uwekezaji, Benki bora ya usimamizi nchini Tanzania, n.k. Zaidi ya hayo, katika kipindi cha miaka 25 tumeweza kutoa michango mbalimbali katika maeneo mengi ya kijamii ikiwemo sekta ya afya na elimu.

Katika jubilei hii ya kipekee, napenda kuwashukuru kwateja wetu na wadau wetu wote kwa mchango wao endelevu na kwa kuipa nafasi benki hii kuwa sehemu ya ndoto zao. Na zaidi tutaendelea kujidhatiti katika kuwasaidia kuona fursa mpya kwa ajili ya kuleta maendeleo jumuishi.

Aidha, tunapoanza kuandika sura nyingine ya miaka 25, naamini kuwa mafanikio yapo karibu kutokana na nguvu na mchango wa pamoja tunaopata kutoka kwa wateja wetu, wadau wetu na watu wa kipekee tulionao ndani ya benki ya Stanbic. Tunatazama mbele kwa mtazamo chanya, hivyo nakukaribisha wewe uweze kuungana nasi katika miaka 25 ijayo na zaidi. Tutaendelea kubaki na kujikita kikamilifu katika wito wetu, 'Afrika ni nyumbani, na sisi ndio tunaoendesha ukuaji wake'.

Wako,

**Kevin Wingfield**
**Mtendaji Mkuu**

Stanbic Bank
A member of Standard Bank Group

# JPM ateta na Rais Nyusi wa Msumbiji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli jana amefanya mazungumzo kwa njia ya simu na Rais wa Jamhuri ya Msumbuji, Filipe Jasinto Nyusi, kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na Msumbiji na ya kikanda.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema Rais Magufuli amempongeza na kumtakia heri Rais Nyusi na wananchi wote wa Msumbiji kwa taifa hilo kuadhimisha miaka 45 ya tangu kupata uhuru wake.

Amemweleza Rais Nyusi kuwa Tanzania itaendeleza ushirikiano na uhusiano mzuri wa kidugu, kirafiki na ujirani mwema na Msumbiji kama ulivyoasisiwa na Baba wa Taifa la Tanzania, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Hayati Samora Mosës Machel wa Msumbiji katika masuala mbalimbali yakiwamo ya kiuchumi na kijamii.

Viongozi hao wamezungumzia maandalizi ya kupokezana kijiti cha uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Rais Magufuli ambaye ni Mwenyekiti wa sasa wa SADC atamkabidhi uenyekiti Rais Nyusi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa SADC kwa sasa.

Viongozi hao pia wamezungumzia ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) na kubadilishana mawazo juu ya namna bora ya kukabiliana na ugonjwa huo, hasa namna Tanzania ilivyofanikiwa kupunguza maambukizi yake.



Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akizungumza na wakazi wa eneo la Mbwawa, katika Mji wa Kibaha, mkoani Pwani na kuwahakikishia kuwa tatizo la maji katika eneo litakwisha ndani ya siku 60. Mradi huo utagharimu kiasi cha Sh. milioni 700 na utatekelezwa na DAWASA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Profesa Mkumbo ajitosa kuwania ubunge Ubungo

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema anatarajia kugombea ubunge katika Jimbo la Ubungo endapo atapitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Jimbo hilo lilikuwa likiongozwa na Mbunge kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Saed Kubenea.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapa alipokuwa akizungumza katika hafla ya utiaji saini kati ya wizara hiyo na Mamlaka za Maji nchini.

Katika hafla hiyo, Prof. Mkumbo alieleza dhamira yake ya kwenda kugombea katika jimbo hilo na kuwaaga watumishi wa wizara hiyo.

"Muda mfupi ujao nitachukua likizo isiyo na malipo kama kanuni zinavyoelekeza kwa ajili ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha ubunge Jimbo la Ubungo naomba watumishi mniombee," alisema.

Akizungumza kuhusu hafla hiyo, Prof. Mkumbo aliwataka wakurugenzi wa mamlaka hizo kudhibiti upotevu wa maji ambao unasababisha upotevu wa mapato ya kiasi cha Sh.bilioni nane kwa mwezi.

"Hili tatizo bado 'we are losing money' na tumefanya 'calculation' kwasababu sasa hivi tunakusanya kwa mamlaka za maji nchi nzima Sh. bilioni 22 kwa mwezi, sasa kiasi hichi uondoe asilimia 40 maana yake tunapoteza mapato takribani Sh. bilioni 8," alisema.

Alisema kiasi cha upotevu wa maji kinachokubalika ni asilimia 20, hivyo kuokoa Sh. bilioni nne kama upotevu huo ungethibitiwa.

"Wenzetu duniani wanapambana sasa hivi kuwa kwenye tarakimu moja kwenye upotevu wa maji, sisi bado tunacheza kwenye asilimia 36 hadi 38, kiasi ambacho bado ni kikubwa," alisema.


Aidha, alisema wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21, imetenga Sh. bilioni mbili kwa ajili ya miradi ya maji vituo vya afya na shule ili kuondoa tatizo sugu la ukosefu wa maji.

Prof. Mkumbo alisema fedha hizo zitasaidia kujenga mifumo ya maji katika maeneo hayo ambayo imeonekana kuna changamoto ya maji jambo

linalorudisha nyuma maendeleo ya taasisi hizo.

"Mimi mwenyewe nimeona katika Kituo cha Afya kimoja wilayani Ikungi wajawazito waende na ndoo ya maji wakati wa kujifungua, That's too bad," alisema Prof. Mkumbo.

Awali akizungumza katika hafla hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, aliwataka kushughulikia malalamiko ya wateja kuhusiana na ankara za maji.



## Mhariri wa siasa Nipashe afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MHARIRI wa makala za siasa, Raphael Kibiriti, amefariki dunia juzi nyumbani kwake Wazo Hill jijini Dar es Salaam baada ya kuugua kwa muda.

Kibiriti aliajiriwa na kampuni ya The Guardian, Aprili Mosi mwaka 2016 na kufanya kazi kwenye gazeti la Nipashe mpaka umauti ulipomfika.

Kabla ya kujiunga na kampuni hiyo, alifanya kazi maeneo mbalimbali ikiwamo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Alilitumikia JWTZ kuanzia mwaka 1988 hadi mwaka 2000 na mwaka 2001 alifanya kazi katika kampuni ya ulinzi ijulikanayo kama Security Group Tanzania na kuondoka mwaka 2006.

Mwaka 2006 alijiunga na Omega Nitro Risk Management hadi mwaka 2008.

Kwa upande wa elimu, Kibiriti alipata Shahada ya Kwanza ya Uandishi wa Habari aliyoisomea kwa muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2011 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alihitimu kidato cha sita mwaka 1988 katika Shule ya Sekondari Mzumbe na kidato cha nne alisoma katika Shule ya Sekondari Kigurunyembe mkoani Morogoro kuanzia mwaka 1982 hadi mwaka 1985.

Marehemu Kibiriti ameacha mke na watoto watatu ambao ni Rogders, Louis na Chesco.

Mke wa marehemu, Lilian Timbuka aliliambia Nipashe jana kuwa, mazishi ya mume wake yanatarajia kufanyika siku ya Ijumaa katika makaburi ya Kota yaliyopo nyumba ya kiwanda cha Wazo Hill baada ya ibada itakayofanyika Kanisa la Katoliki Wazo kuanzia saa 7:30 mchana.

Alisema mwili utafika nyumbani saa 5:00 asubuhi na baada ya chakula cha mchana ndipo utaelekea kanisani.

Msiba upo nyumbani kwake maeneo ya Wazo Mafuriko karibu na Zahanati ya Wazo Hill.

Bwana alitoa, Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe, pumzika kwa amani, Raphael Kibiriti.

# Ufaransa yamwaga mil. 780/- kudhibiti magonjwa ambukizi

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Huduma za Afya Aga Khan wametia saini makubaliano ya ruzuku ya Euro 300,000 (sawa na Sh. milioni 780) ili kufungua vitengo vya magonjwa yanayoambukiza katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.

Makubaliano hayo yalifanyika jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Huduma za Afya Aga Khan Kanda ya Afrika Mashariki, Sulaiman Shahabuddin, na Mkurugenzi Mkazi wa AFD nchini, Stéphanie Mouen.

Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo, Shahabuddin alisema ruzuku hiyo itawezesha kuimarisha mfumo wa sasa ili kushughulikia changamoto zinazohusiana na usimamizi wa udhibiti wa magonjwa hayo.

"Itaiwezesha Aga Khan kuitikia vya kutosha suala la magonjwa-tandavu, kama vile corona, ikiwamo kushughulikia uhaba wa miundombinu na uwezo wa huduma za afya," alisema Shahabiddin.

Alisema wanaamini kitengo hicho kitaunga mkono jitihada za serikali katika kupunguza usambaaji wa magonjwa yanayoambukiza na kusaidia kudhibiti magonjwa-tandavu.

"Ruzuku hii inatolewa kama sehemu ya mpango wa kimataifa unaojulikana kama 'COVID 19- Health in Common' ulioanzishwa na Rais wa Ufaransa na kutekelezwa na AFD kama mwitikio wa janga la kidunia la afya ya umma linalosababishwa na magonjwa-tandavu yanayoenea duniani kote," alisema.

Naye Mouen alisema ahadi za masuala ya kijamii zilizotolewa na Aga Khan zilikuwa chachu wa uamuzi wa AFD wa kushiriki kufadhili mpango huo.

"AFD inaamini kwamba mpango huu utadhihirisha mwitikio na ufanisi wake katika kuunga mkono maendeleo ya wabia wetu hasa katika kanda ya Afrika Mashariki ili kuleta matokeo yanayotarajiwa," alisema.




Wajumbe wa timu ya kampeni ya 'Mikono Safi Tanzania Salama' wakiwa wameshika bango lenye ujumbe wa kujikinga na ugonjwa wa corona, katika maonyesho ya barabarani, mkoani Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi wa miundombinu Dar wamridhisha Makonda

**Fatma Mtutuma na Faudhia Sultan, UDOM**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema kuwa ujenzi wa barabara kilomita 111 kwa kiwango cha lami na kilometa 40 ya mito na mabonde ya kilometa 150, umefikia hatua nzuri.

Akizungumza na wananchi wa kata ya Sinza, jijini Dar es Salaam, baada ya kufanya ziara ya kukagua miundombinu hiyo, alisema ameridhishwa na ujenzi huo.

Aidha, alisema serikali ilitenga zaidi ya Sh. trilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara, vivuko na kutengeneza mito na mabonde katika Wilaya ya Ubungo na majimbo yake.

"Hizi ni barabara mpya za lami na siyo changarawe wala vumbi, pia kuna kilometa 40 za kutengeneza mito na mabonde kwa ajili ya watoto kuvuka wakati wanapotoka shule," alisema Makonda.

Alizitaja barabara hizo kuwa ni Kigogo, Aseno Magoti, Kata ya Saranga na Kata ya Kimara ni za Kibanda cha Mkaa, Temboni, Stopover, Suka, Baruti na Kilungule.

Kadhalika alisema anamwamini Rais Magufuli kwa uchapaji wake wa kazi na anatumaini atachukua urais kwa nafasi nyingine kwa ajili kuendelea kuboresha maendeleo ya nchi.

Naye, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, ambaye ni mlezi wa CCM Dar es Salaam, Zakaria Mwasasu, alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kusimamia maendeleo ya mkoa huo ambayo yameleta mafanikio katika maisha ya wananchi.

# Ardhi kinara wa rushwa Dodoma

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SEKTA ya ardhi mkoani Dodoma imetajwa kuwa kinara wa vitendo vya rushwa kwa asilimia 25 katika kipindi cha miezi mitatu.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2020(Aprili hadi Juni) kwa mkoa huo.

Kibwengo alisema kwa upande wa serikali za mitaa vitendo vya rushwa ni asilimia 17 huku Vyama vya Ushirika vikiwa na asilimia 16.

Alisema rekodi hiyo sio nzuri katika sekta muhimu kama hizo, na kuwataka watendaji wa maeneo hayo waache tabia ya kuchukua rushwa kwa kuwa Takukuru ipo kila kona kusaka wanaofanya vitendo hivyo.

Aidha, alisema nafasi ya nne kwa rushwa imeshikwa na sekta ya Elimu kwa asilimia nane huku sekta ya Afya, Ujenzi na Mahakama zikiwa na asilimia saba, kila moja na Polisi ni asilimia sita.

Alisema Takukuru wanaendelea na uchunguzi katika sekta hizo ambazo zinaendeleza vitendo vya rushwa dhidi ya utendaji wao.

Aliwakumbusha viongozi wa maeneo hayo ambayo yanalalamikiwa zaidi hasa yale ambayo ni vinara wa vitendo vya rushwa wachukue hatua ya kuboresha mifumo yao ili kudhibiti vitendo vya rushwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA UMMA**

**UFAFANUZI JUU YA UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA KURASIMISHA UMILIKI WA LAINI ZA SIMU ZAIDI YA MOJA KATIKA MTANDAO MMOJA**

**1.0 UTANGULIZI**

Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Usajili wa Laini za Simu) za mwaka 2020, yaani "The Electronic and Postal Communications (SIM Card Registration) Regulations, 2020", zimeainisha katika Kanuni ya 18 kuwa:-

18 (1) Mtu anayehitaji kumiliki na kutumia laini ya simu ataruhusiwa kusajili:-

(a) Kama ni mtu binafsi
i. Idadi ya laini moja kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa ajili ya kupiga simu za sauti, kutuma ujumbe mfupi pamoja na matumizi ya data;
ii. Idadi ya laini zisizozidi nne kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa matumizi ya mawasiliano kati ya mashine na mashine; na

(b) Kama ni Kampuni au Taasisi
i. Idadi ya laini zisizozidi thelathini kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa ajili ya kupiga simu za sauti, kutuma ujumbe mfupi pamoja na matumizi ya data;
ii. Idadi ya laini zisizozidi hamsini kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa matumizi ya mawasiliano kati ya mashine na mashine.

(2) Laini zilizosajiliwa kwa matumizi yaliyoainishwa kwenye Kanuni 18 (1) (a) hazipaswi kutumiwa kwa kubadilishana (interchangebly).

(3) Bila kujali Kanuni ya 18 (1), Mtu binafsi, Kampuni au Taasisi inaweza kuruhusiwa kusajili na kumiliki laini zaidi ya zilizoainishwa kwa kuomba na kupata idhini kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi, atakuwa ametenda kosa la jinai.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu umma kwamba zoezi la kuomba idhini ya umiliki wa laini za simu zaidi ya moja katika mtandao mmoja linaendelea. Tunawashauri wamiliki wa laini za mawasiliano ya simu kuendelea kuhakiki usajili wa laini zao zote wanazomiliki.

**2.0 KUTHIBITISHA IDADI YA LAINI ZILIZOSAJILIWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIDA)**

2.1 Kila mmiliki wa laini ya simu anatakiwa kupiga namba *106# na kuangalia usajili wa laini anazomiliki na endapo atakuta namba ambayo haitambui na imesajiliwa kwa kutumia namba ya kitambulisho chake cha Taifa anashauriwa kuwasiliana na mtoa huduma wake ili azifunge mara moja kuepusha matumizi mabaya na kumsababishia usumbufu usiokuwa wa lazima utakaojitokeza.

2.2 Kwa wale ambao kwa sasa wanamiliki laini zaidi ya moja katika mtandao mmoja, mwisho wa kuhakiki laini zao itakuwa **tarehe 31 Julai 2020.**

2.3 Utaratibu wa kuomba idhini ya kumiliki laini mpya za ziada katika mtandao mmoja unaendelea na mteja anaweza kupata huduma hii kupitia kwa wakala au kwenye ofisi za watoa huduma ambapo kwa kutumia njia za kielektroniki mtoa huduma atawasilisha maombi ya mteja wake TCRA kwa idhini ya kusajili na kumiliki laini za ziada; mteja atapokea majibu ya maombi yake ndani ya takribani dakika tano.

**3.0 URASIMISHAJI WA LAINI ULIZOTHIBITISHA**

3.1 Urasimishaji wa laini za ziada kwa sasa unaweza kufanyika kwa wakala au kwenye ofisi za watoa huduma ambapo kwa kutumia njia za kielektroniki ambapo mtoa huduma atawasilisha maombi yake ya idhini ya kurasimisha laini za ziada TCRA na kupokea majibu ndani ya takribani dakika tano; au

3.2 Kwa kupitia namba ***106#** ambapo wewe mwenyewe utaweza kuomba idhini ya kurasimisha kutoka TCRA kupitia simu yako. Huduma hii ya kurasimisha kwa njia ya simu yako itaanza kutumika rasmi **Agosti 1, 2020.**

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA),**
**Jengo la Mawasiliano,**
**Kitalu Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,**
**S. L.P 474,**
**14414 DAR ES SALAAM**
**1 Julai, 2020**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Shule binafsi ziache ukaidi kwa serikali

NI jambo linaloshangaza kuona shule nyingi za binafsi nchini zikiwalazimisha wazazi na walezi kulipa malipo ya ziada kwa kisingizio cha ugonjwa wa corona.

Shule hizo zinakaidi kuzingatia maelekezo yote yaliyotolewa na serikali siku chache kabla ya kufunguliwa kwa shule zote baada ya likizo ya dharura iliyoanza Machi 17, mwaka huu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, alizielekeza bodi za shule kuhakikisha zinatumia busara katika kudai ada baada ya shule kufunguliwa Jumatatu, na kwamba wazazi na walezi wasilazimishwe kulipa malipo ya ziada, kwa kisingizio cha ugonjwa huo.

Profesa Ndalichako alitoa maelekezo hayo baada ya wazazi na walezi wengi kulalamikia masharti yaliyowekwa na shule, ambayo yalionekana dhahili kwenda tofauti na malipo rasmi ambayo yanajulikana.

Ujumbe ambao wazazi walikuwa wanatumiwa na shule kuhusu masharti ya kuzingatia, unatoa tafsiri kwamba wamiliki wengi wa shule binafsi wanataka kuwatoza wazazi na walezi malipo ya ziada ili kufidia hasara ambayo waliipata wakati wote ambao shule zilifungwa, hivyo kukosa vyanzo vya mapato.

Kufungwa kwa shule maana yake ni kuwa shule zilikosa vyanzo vya mapato na kujikuta zikishindwa kulipa gharama za uendeshaji zikiwamo mishahara ya walimu na wafanyakazi pamoja na mambo mengine.

Hata hivyo, shule kukosa mapato hakuwahusu wazazi na walezi, hivyo, ni jambo lisilokubalika kwa wamiliki wa shule binafsi kulazimisha malipo ya ziada.

Wengi bila shaka tumeona na kusikia jinsi ambavyo baadhi ya shule kuanzia Jumatatu zilivyowashupalia wazazi na walezi kulipa papo hapo malipo yote waliyokuwa wakidaiwa bila kutumia utu na busara.

Kwa mfano, baadhi ya shule zilikataa kuwapokea wanafunzi ambao hawakukamilisha malipo hata kama walipungukiwa kiasi kidogo, walirejeshwa nyumbani.

Sisi hatukubaliani hata kidogo na shule ambazo zimeamua kwa makusudi kukaidi maelezo ya serikali, badala yake zilipaswa kutumia busara kwa kuwasikiliza wazazi na walezi ambao kwa mamna moja au nyingine hawakukamilisha baadhi ya malipo ili wakubaliane muda wa kuyakamilisha.

Kutoa elimu hakumaanishi kwamba lengo ni kupata fedha zinazolipwa na wazazi na walezi, hivyo shule binafsi nazo zinapaswa kufahamu kuwa zinawajibika kwa jamii.

Tunasema hivyo, kwa sababu zimekuwa zikinufaishwa na jamii, ikiwamo serikali kuziwekea mazingira bora ya kutoa elimu kwa watoto wa kitanzania.

Tunazishauri shule zote zilizokaidi maelekezo ya serikali zijirudi, vinginevyo serikali isione aibu wala huruma kuzichukulia hatua.

Zikumbuke kuwa serikali ndiyo iliyozipatia usajili, na ndiyo yenye sera, kanuni, miongozo na maamuzi yote yanayohusu sekta ya elimu nchini.

Tumefarijika juzi kusikia agizo la Waziri Ndalichako la kupiga marufuku wamiliki wa shule binafsi kutaka kutoza malipo ya huduma ambazo hawakuzitoa kwa wanafunzi wakati wa mlipuko wa corona.


Alisema kuwa serikali ndiyo iliyotangaza kuzifunga shule zote baada ya mlipuko wa virusi vya corona na yenyewe ndiyo imetangaza kuzifungua, hivyo wamiliki wa shule hizo wanapaswa kutii amri hiyo ya Rais John Magufuli.

Tunatarajia shule zilizokataa kupokea wanafunzi zinabatilisha uamuzi huo na kuweka uwazi masuala yote ya ada na malipo mengine yanayojulikana kwa wazazi na walezi.

Kwa upande wa serikali, ni matarajio yetu kwamba itazifuatilia kwa karibu shule zote kuhakikisha maagizo na maelekezo yake yanaheshimiwa na kutekelezwa na wahusika inavyopaswa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Daladala zisijisahau na ruksa shule katika kukabili corona

JUMATATU wiki hii, shule za msingi na sekondari zilifunguliwa ili kuruhusu wanafunzi kuendelea na masomo, baada ya kukaa nyumbani kwa zaidi ya miezi mitatu, kwa lengo la kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Hiyo ni baada ya serikali kutangaza kwamba, hali ya ugonjwa wa corona imeendelea vizuri na hivyo wameamua kuwaruhusu wanafunzi kurudi shuleni Juni 29, ili vijana na watoto waendelee na masomo.

Pamoja na kuruhusu shule kufunguliwa, msisitizo ukawa ni kuwasihi Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari na pia kuzingatia ushauri unaotolewa na wataalamu wetu wa afya, kwa vile ni muhimu kuzingatia hilo.

Lakini, inaonekana ruhusa hiyo ya serikali imechukuliwa vibaya na baadhi ya makondakta na madereva wa daladala, ambao tangu Juni 29, wamekuwa wakijaza abiria kama zamani kabla ya corona.

Ikumbukwe, Watanzania wanaendelea kusisitiziwa kuchukua tahadhari na kuzingatia ushauri wa wataalamu wetu wa afya, hasa kunawa mikono kwa maji tiririka, kuvaa barakoa na ukaaji wa 'level seat' katika daladala.

Hatua ya daladala kubeba abiria kwa idadi ya viti 'level seat' ulikuwa ni mkakati wa kupambana na kuenea kwa virusi vya corona. Utaratibu huo ulianza Machi 31 mwaka huu.

Ubebaji huo una changamoto zake, kwani wakati unaanza, kwenye vituo mbalimbali vya daladala, mamia ya abiria walikosa usafiri, daladala nyingi zilifika vituoni, zikiwa zimeshajaa abiria.

Hata hivyo, serikali iliamua kuruhusu magari binafsi kuomba vibali vya muda kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na hadi sasa yanaendelea kutoa huduma. Kimsingi, yamesaidia kupunguza mrundakano wa abiria vituoni.

Lakini jambo la kushangaza ni kwamba, tangu shule kufunguliwa, imekuwa kama daladala nazo zimefunguliwa kubeba abiria kupita kiasi kama zamani kabla ya tishio la virusi vya corona.

Yaani wahusika wamejisahau, badala ya kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya yakiwamo ya kukaa umbali wa mita moja, sasa wajazana katika daladala.

Sidhani kama kufunguliwa kwa shule ilikuwa ni ruhusa kwa daladala kuanza kubeba abiria kupita kiasi, kwani pamoja na kuruhusu masomo kuendelea, msisitizo ulikuwa watu kuendelea kuchukua tahadhari.

Hivyo sasa ni vyema wale ambao wamejisahau, wakumbuke kuwa kuna haja ya kuchukua tahadhari na siyo kweli kwamba kufunguliwa shule, kumeenda sambamba na kuruhusu kujaza abiria katika daladala.

Abiria hawana budi kujiongeza na kuacha kujazana, badala yake wachukue tahadhari kwa ajili ya usalama wa afya zao, wakiona daladala imejaa, waachane nayo na kusubiri nyingine.

Ninaamini kwamba wakizingatia utaratibu wa kubeba abiria kulingana na idadi ya viti, huku wakisimamisha wanafunzi wa nne kama, ambavyo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliagiza, kutakuwa na usalama.

Kimsingi ni kwamba, jamii isizembee mambo ya msingi kama hayo yanayolenga kulinda afya, vinginevyo ni sawa na kusababisha matatizo na kwamba hakuna tahadhari.

Madereva, makondakta na abiria, kila mmoja azingatie tahadhari iliyotolewa na serikali, kwani itakuwa na faida gani kama watajaza abiria kupita kiasi na mwisho wa siku wakajikuta wameambukizwa corona?

Abiria nao watakuwa na faida gani kutaka kuwahi kwenye shughuli na kulazimika kupanda daladala iliyojaa, halafu mwisho wa siku wajikuta wanaambukizana corona? Chukueni tadhadari!

Ni kweli, maisha lazima yarudi na yaendelee kama yalivyokuwa zamani, lakini kuchukua tahadhari ni jambo la muhimu kwa mustakabali wa afya ya kila mmoja wetu, kuliko kujiendea kienyeji tu.

Kama wahusika watashindwa kujiongeza, ili kuzingatia tahadhari, basi wahusika askari Polisi, Trafiki, waingilie kati kukamata daladala zilizosimamisha abiria na kuwashusha kwa lengo la kuendelea kudhibiti kuenea virusi vya corona.

Wakishushwa huku madereva na makondakta wakichukuliwa hatua zaidi za kisheria, hatua hiyo inaweza kusaidia kuendelea kupunguza kama siyo kumaliza kabisa tishio la virusi, hivyo kwenye usafiri.

# Wanasiasa watakiwa kujifunza kujenga hoja

**Na Mary Geofrey**

VIONGOZI wa vyama vya siasa nchini, wametakiwa kutotumia lugha ya matusi na badala yake kujibizana kwa hoja ili kujenga demokrasia nchini.

Wito huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohamed Ali Ahmed, wakati akifunga kikao cha viongozi wa siasa na ofisi ya msajili kilichokuwa na lengo la kujadili maadili kwa viongozi.

Alisema demokrasia ya kweli inajengwa kwa hoja na sio majibizano ambayo hayana msingi, kama ambavyo wanafanya baadhi ya viongozi.

Ahmed alisema ofisi yake ina dhamana kubwa ya ulezi na kuvifanya vyama vya siasa kujiendesha vizuri ili kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema walifanya kikao hicho mahususi kwa ajili ya kutoa mafunzo na kusikiliza changamoto mbalimbali ili kuendelea kujenga ushirikiano.

"Nawashukuru kwa muitikio huu inaonyesha ni kwa namna gani mlikuwa mnasubiri elimu hii. Ni vyema mkaitumie vizuri na tutaamini tumefikia ile adhma yetu ya kuhakikisha tunavijengea uwezo vyama vyote kuwa safi na imara ili kuingia katika uchaguzi mkuu tukiwa vizuri," alisema Ahmed.

Naye, Katibu Mkuu ADC, Doyo Hassan, alisema alipongeza Ofisi ya Msajili kwa kuandaa kikao hicho ambacho kilikuwa na malengo ya kuwaweka pamoja na kufanya siasa za kistarabu.

Naye, mwanasiasa Mkongwe, Anna Abdallah, alishukuru Ofisi ya Msajili kwa kuwakutanisha viongozi hao kwa sababu wanapokutana na kuzungumza wataweza kufika mbali.

"Awali tulikuwa tunanyoosheana vidole kwa kulaumiana, ila Msajili ametukutanisha na kumaliza suala hili kwa njia nzuri ambayo itasaidia kutujenga sisi wote," alisema Abdallah.

Alisema wanasiasa wanatakiwa kuacha kudhani kuwa siasa ni ugomvi bali ni jambo ambalo linaleta maendeleo.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam, Rostam Kamazi (kulia), akilipia huduma ya Bima kupitia wakala Esther Barnaba katika Banda la Benki ya NMB, kwenye maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa yaliyoanza katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Likizo corona yaibua wanafunzi 40 wajawazito

**Na Ambrose Wantaigwa, BUNDA**

SERIKALI wilayani Bunda, mkoani Mara imeanzisha msako wa watuhumiwa wa ubakaji na kuwapa ujauzito wanafunzi zaidi ya 40.

Hali hiyo ya wanafunzi kupata ujauzito imegundulika wakati walipoanza kuripoti shuleni kuanzia wiki hii katika hatua ya msingi na sekondari baada ya likizo ya corona.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alisema wakati akipokea ripoti ya utekelezaji wa ilani ya serikali, kuna wasiwasi idadi hiyo ikaongezeka.

Alisema kuanzia mwezi Januari hadi Juni, mwaka huu wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 26, walipata ujauzito, huku matukio mengine 19 ya ubakaji yakiripotiwa wilayani hapa.

"Serikali imeanzisha msako mkali kwa wale wote waliohusika na unyanyasaji huu kwa namna moja au nyingine wakiwamo wazazi wanaodaiwa kuwaozesha mabinti hao na kupokea mahari," alisema Bupilipili.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 80 imetekelezwa wilayani hapo ikiwamo ya elimu, afya, barabara na maji.

Kulingana na asasi za kiraia zinazotetea haki za wanawake na watoto wilayani humu, sababu zinazohusishwa na kuongezeka kwa matukio ya ukatili huo wa watoto ni pamoja na imani za kishirikina na umaskini.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Kivulini, Yassin Ally, alisema asasi hiyo imefadhili masomo ya mtoto mmoja aliyedaiwa kubakwa na baba yake mzazi hadi ngazi ya chuo kikuu.

# TCRA yatoza mil. 48/- vyombo vya habari

**Na Mary Geofrey**

KAMATI ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetoa adhabu ya faini ya Sh. milioni 48 na onyo kwa vituo vya utangazaji tisa zikiwamo blog, televisheni na redio.

Vituo hivyo vimepewa adhabu hizo kwa makosa ya kukiuka Kanuni za Mawasiliano na Posta za mwaka 2018 na kukiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta ya mwaka 2018.

Akisoma hukumu hiyo jana jijini Dar es Salaam kwa waandishi wa habari, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui wa TCRA, Joseph Mapunda, alisema vituo hivyo vilitenda makosa hayo kati ya Februari hadi Juni mwaka huu.

Alisema vyombo hivyo baada ya kutenda makosa tofauti tofauti vilitakiwa kuwasilisha utetezi wa maandishi na baadaye utetezi wa maongezi ambao hata hivyo, haukuiridhisha kamati hiyo ishindwe kutoa adhabu iliyotoa.

Mapunda alisema kuna vyombo vilitakiwa kuomba radhi kupitia vipindi vyao kwa makosa waliyofanya, vingine vimefungiwa kuchapisha maudhui kwa muda, vilipewa onyo na adhabu ya faini kwa ajili ya kudhibiti ukiukwaji wa kanuni hizo.

Kadhalika, vyombo hivyo vilitakiwa kutoendelea kurudia makosa waliyotenda vinginevyo watapewa adhabu kali zaidi.

Aidha, alivitaka vyombo vya utangazaji ambavyo havijaridhika na adhabu zilizotolewa kukata rufani ndani ya siku 21.

**Mapunda alisema kuna vyombo vilitakiwa kuomba radhi kupitia vipindi vyao kwa makosa waliyofanya, vingine vimefungiwa kuchapisha maudhui kwa muda, vilipewa onyo na adhabu ya faini kwa ajili ya kudhibiti ukiukwaji wa kanuni hizo.**

# Katibu Mkuu awabana waganga wakuu mikoa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia masuala ya afya, amewataka waganga wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuhakikisha ndani ya siku saba wanaimarisha mfumo wa huduma kwa wateja, ili wananchi wawasilishe kero zao mahali sahihi na kupatiwa ufumbuzi kwa wakati.

Dk. Dorothy Gwajima, alitoa agizo hilo jana katika ziara yake ya kikazi ya kukagua uimarishaji mfumo huo kwenye Hospitali za Mnazi Mmoja na Sinza Palestina jijini Dar es Salaam.

Alisema amebaini uwapo wa baadhi ya watumiaji wa huduma za afya katika baadhi ya vituo kulalamikia kero walizokutana nazo wakati wa kupata huduma za afya ambazo ni za muda mrefu, lakini zimekosa ufumbuzi kwa wakati.

Alisema kila zahanati, kituo cha afya na hospitali ya halmashauri lazima iwe na bango kubwa lenye kuonyesha namba maalum ya simu ya kituo kwa ajili ya kushughulikia kero za wateja wanaofika kupata huduma za afya.

"Pia, namba ya Mganga Mfawidhi wa Kituo husika, namba ya Mganga Mkuu wa Halmashauri, Mganga Mkuu wa Mkoa, namba za Ofisi ya Rais Tamisemi na namba ya kituo maalum cha simu cha Wizara ya Afya ambayo ni 199 ziwapo kwenye bango," aliagiza.

Alitoa wito kwa watumiaji wa huduma za afya nchini, kutumia namba za huduma kwa wateja zilizoko katika vituo hivyo, ili kuwasilisha kero zao mahali sahihi na kupatiwa ufumbuzi kwa wakati.

"Ili kuhakikisha kero hizo zinafika kwa wakati, kila kituo cha kutolea huduma za afya (zahanati, kituo cha afya na hospitali ya halmashauri) lazima kuimarisha mfumo mzima wa huduma kwa wateja kwa kutumia utaratibu wa kuweka namba za simu kwenye eneo la wazi linaloonekana," alisisitiza.

Dk. Gwajima alibainisha kuwa lengo la kuimarisha huduma kwa wateja ni kutatua kero zao kwa wakati na kuhakikisha kila mwananchi anayefika kwenye kituo cha huduma za afya ngazi ya msingi, anafurahia huduma hizo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alisema kuwa kwa kushirikiana na watendaji wenzake ndani ya mkoa huo, ndani ya siku saba watakuwa wametekeleza agizo hilo.



Mbuzi wakisaka chakula kwenye takataka zilizotelekezwa bila ya kuzolewa kando ya Barabara ya Kilwa, eneo la Mtoni kwa Aziz Ally, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TFS yahadharisha wakulima

**Na Sara Magesa, Chato**

WAKALA wa misitu nchini (TFS), imewataka wakulima wanaoandaa mashamba kwa msimu wa kilimo kwa kuchoma moto, kuwasiliana na wataalamu wa misitu waliopo kwenye maeneo yao ili kuepukana na janga la moto.

Mtaalamu wa kufuatilia moto wa msituni kwa njia ya setilaiti kutoka TFS, Kekilia Kabalimu, aliyasema hayo jana wakati wa kutoa elimu ya kuzuia majanga ya moto msituni kwa watumishi wa TFS kutoka mikoa ya Kagera, Mwanza na Geita.

Elimu hiyo ilitolewa pia kwa wakazi wanaozunguka shamba la miti Biharamulo.

Alisema kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa, Kanda ya Ziwa ipo kwenye hatari zaidi kukumbwa na majanga ya moto katika msimu huu na ndiyo maana TFS inatoa elimu ya namna ya kuzima moto.

"Eneo likiwa kwenye hatari ya moto hata mtu akitupa kipande cha sigara ni rahisi kusababisha janga la moto ndio maana tumeamua kutoa elimu kwa watumishi wetu, ili waweze kufuatilia maeneo yenye hatari kwa njia ya setelaiti na kuuzima mapema," alibainisha Kabalimu.

Alisema shughuli za kibinadamu zinazofanywa bila kuzingatia tahadhari ya mapema ya moto imesababisha zaidi ya hekta milioni 10 kuunguzwa moto mwaka 2019, na kwamba mikoa inayoongoza kwa uchomaji moto ni Katavi, Tabora na Kigoma.

Alisema elimu ya tahadhari ya mapema imesaidia kupunguza vitendo vibaya vya moto kwa asilimia 55 na kusema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni vitendo haramu vinavyofanywa na wafugaji wanaochoma mashamba kiholela ili mimea iweze kuchipua upya.

Naye, Innocent Charles mkazi wa Butengorumasa wilayani Chato, alisema mafunzo ya namna ya uwashaji na uzimaji moto na namna ya kuandaa shamba yatawasaidia kuandaa shamba kitaalamu na kuuzima wakati wa kuandaa shamba.

# Miundombinu ya TANESCO yapeleka wawili jela miaka 12

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imewahukumu watu watatu kwa kosa la kuingilia miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Waliohukumiwa ni mafundi umeme wawili Jiddah Abdallah na Abel Myonga kwenda jela miaka 12 na mwenye nyumba Hashim Rwambo kulipa fidia ya Sh. milioni mbili.

Hata hivyo, hukumu hiyo ilisomwa huku washtakiwa wakiwa wameruka dhamana.

Hukumu hiyo ilisomwa na Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabati.

Alisema baada ya kusikiliza ushahidi mahakama bila kuacha shaka imewaona washtakiwa wana hatia ya makosa ya kuingilia miundombinu na kuiharibu.

Alisema mshtakiwa wa kwanza na wa pili watakwenda jela miaka 12 na mshtakiwa wa tatu atalipa fidia ya Sh. milioni mbili.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa siku isiyofahamika, mshtakiwa wa kwanza na wa pili, Agosti, 2016 eneo la Mbezi Juu Goba kwa Sanya waliingilia miundombinu ya umeme kwa kumuunganishia umeme mshtakiwa wa tatu Rwambo.

Shtaka la pili, ilidaiwa siku ya tukio la kwanza washtakiwa waliharibu miundombinu kwa kuunganisha umeme uliokuwa ukitoa huduma muhimu.

Kosa la tatu wanadaiwa kuisababishia serikali hasara ya Sh. 2,114,228.26 kwa makusudi.

# Aenda jela miaka 13 kwa kuiba pikipiki

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu mkazi wa Kata ya Mnazi-Mmoja, Rahimu Mohamedi Mbongo (Tongolanga), kifungo cha miaka 13 gerezani baada ya kupatikana na kosa la wizi wa kuaminika wa mali zenye thamani ya Sh. 6,620,000 kutoka kwa watu tafauti.

Hukumu hiyo ilitolewa kwa nyakati tafauti na mahakimu Maria Batraine na Muyonga Magala, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri, ambapo wizi huo unaelezwa kufanywa mwaka 2019 na 2020.

Mshtakiwa Rahimu alikabiliwa na kesi tatu namba 14,15 na 16/2020, zote zinahusu wizi wa pikipiki,zikiwamo mbili aina ya Sanlg na nyingine TVS zenye thamani ya Sh. 6,622,000, mali za Erick Joel Nyakata, Ally Mohamedi Alimisi na Wasonga Madieni.

Hakimu Maria Batraine akitoa adhabu dhidi ya Rahimu Mbongo kupitia kesi namba 14 na 15/2020, kupitia kifungu cha 273 (b) kanuni ya adhabu sura namba 16/2002, kifungo cha Jumla ya miaka 10 kwa kila kesi miaka mitano na atakapomaliza alipe Sh. 4, 550,000 kama fidia kwa Pikipiki alizoiba.

Nae,Hakimu Muyonga Magala akitoa hukumu katika kesi namba 16/2020,inayomuhusu mshitakiwa huyo huyo kupitia kifungu hicho hicho ,alimhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitatu gerezani na akimaliza kifungo alipe fidia ya Sh. 2,070,000.

Kwa kuwa adhabu hizo zinajitegemea, mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka 13.

## HABARI KITAIFA

# Kichocheo cha kasi ya matukio udhalilishaji wa kijinsia hiki

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JUMUIYA ya Tumaini Jipya Pemba 'Tujipe' imesema rushwa muhali na mashahidi kutokwenda mahakamani kutoa ushahidi, ndio janga baya zaidi katika jamii.

Imeelezwa kuwa rushwa hiyo ni mbaya zaidi kuliko hata vitendo vya udhalilishaji.

Mratibu wa Jumuiya hiyo, Tatu Abdalla Mselem, alisema serikali kwa nia nzuri, ilizifanyia marekebisho sheria za ushahidi, sheria ya adhabu na ya mwenendo wa makosa ya jinai na kuweka adhabu kali kwa wakosaji, lakini hayo yote yanategemea jamii kutoa ushahidi.

Akizungumza kwenye mkutano wa masheha, waratibu wa wanawake na watoto wa shehia za Matale, Pujini, Uwandani, Mchanga Mrima na Wara Wilaya ya ChakeChake, wanasheria, watendaji wa kituo cha mkono kwa mkono na madawati, alisema, uwapo wa sheria kali ni jambo moja na utekelezaji ni jambo jingine.

Alisema, majaji, mahakimu, waendesha mashtaka, polisi na mawakili hawawezi kufanya jambo lolote ikiwa rushwa muhali itatawala katika jamili.

Aliwasisitiza masheha na waratibu wa shehia hizo, kuendelea kuwaelimisha wananchi na hasa waathirika wa matukio ya udhalilishaji ili wasiache kufika mahakamani kutao ushahidi na kukataa suluhu.

"Hapa lazima tujiulize sisi wanajamii tumekosea wapi, maana zamani ilikuwa tukilalamika adhabu ndogo kwa wakosaji... sasa kuna adhabu kali wanajamii hawafiki mahakamani kutoa ushahidi na wengine hupokea hata rushwa, jambo hili sio sahihi," alieleza.

Katika hatua nyingine mratibu huyo alisema jumuiya yao imekuwa ikitafuta ufadhili kila kona kuhakikisha inaisaidia jamii ya Pemba katika kutokomeza vitendo vya udhalilishaji.

Hata hivyo, aliwasisitiza wanasheria wanaoendesha kesi za udhalilishaji, kuhakikisha wanazitumia sheria kama zilivyo ili wanaotiwa hatiani wasirudie kutenda makosa hayo.

Katibu wa Jumuiya hiyo, Ibrahim Omar Mohamed, alisema makosa ya udhalilishaji ni rahisi kutokomezwa Zanzibar ikiwa kila mmoja atatekeleza wajibu wake na rushwa kwake kuwa mwiko.

Alieleza kuwa iwapo jamii itaachana na rushwa muhali na kufika mahakamani kutoa ushahidi, na mahakimu na waendesha mashtaka kutimiza wajibu wao, matendo hayo yanaweza kuwa historia.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Pemba, Juma Ali Juma, akiwasilisha mada ya ukatili na unyanyasaji wa wanawake na watoto, alisema dawa ya kuyaondoa matendo hayo na jamii kutoa ushahidi mahakamani.

Sheha wa Shehia ya Matale, Mkubwa Hamad Hassan, alisema wakati umefika kwa vyombo vya sheria kuacha kukinzana kisheria juu ya aina ya adhabu kwa washtakiwa wa makosa hayo.

Naye Ofisa Mipango Wilaya ya Chakechake, Kassim Ali Omar, alisema changamoto zinapokuwa nyingi kuanzia ngazi ya jamii hadi kwenye utekelezaji wa sheria kwenye mahakama na polisi, inaipa shida jamii kuamini kuwa kuna siku matendo hayo yanaweza kuondoka.



Mfanyabiashara mdogo maarufu machinga, akibomoa kibanda chake cha biashara Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, ili kupisha upanuzi unaoendelea wa barabara ya Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mradi wa maji wa bil. 30/- wanufaisha wakazi Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya, MBINGA**

WAKAZI wa Mkoa wa Ruvuma wananufaika na utekelezaji wa miradi ya maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 30 zilizotolewa na serikali ili kuwaondolea kero ya maji wananchi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, wakati anakagua mradi wa maji wa Myangayanga Wilaya ya Mbinga, ambao serikali inautekeleza kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 284.

Mndeme aliwaomba wakazi wa Wilaya ya Mbinga kutunza chanzo cha maji cha Miyangayanga chenye uwezo wa kuhudumia watu zaidi ya 12,000 na kinaweza kutoa lita 200,000 za maji.

"Asante pekee ambayo tunaweza kumpa Rais wetu ni kutunza mazingira tusifugie kwenye chanzo cha maji, tusilime wala kukata miti, Mbinga hatujajaa," alisema Mndeme na kuongeza:

"Tunataka maji haya yanayopatikana katika chanzo hiki yahudumie wakati wa masika na kiangazi bila kupungua."

Naye Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mbinga, Mashaka Sinkala, alisema Mamlaka hiyo imepanga kujenga mtandao wa mabomba wa njia kuu hadi kwenye tenki umbali wa kilomita 4.4.

Alisema RUWASA, Wilaya ya Mbinga itaanzisha jumuiya ya maji ngazi ya jamii itakayokuwa na jukumu la kusimamia na kuendesha mradi kwa mujibu wa Sheria ya Maji Namba 5 ya 2019 pamoja na kanuni zake za uanzishwaji wa jumuiya hizo.

Amesema chanzo hicho cha maji ya mserereko kina uwezo wa kuzalisha maji zaidi ya lita za ujazo 300,000 na kinaweza kutosheleza watu zaidi ya 12,000, na kwamba mradi ukikamilika kwa kuanzia utahudumia watu 2,300.

## Wakazi Kimara walalamikia kukithiri matukio ya uhalifu

**Na Magdalena Haule**

WAKAZI wa Kimara Vyumba Nane jijini Dar es Salaam wamelalamikia kukithiri kwa matukio ya wizi na ukabaji katika makazi yao hasa usiku.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wakazi hao, David Amos, alisema matukio ya wizi na ukabaji yamekuwa tishio kubwa katika maeneo yao husasan usiku.

''Kwa sasa katika maeneo yetu tunaibiwa sana, watu wengi wanalalamika kuibiwa, juzi juzi wamekata nyavu za dirishani kwangu, lakini hawakufanikiwa kuchukua chochote... jana kuna mdada usiku aliporwa simu na wezi hao walikimbia," alisema Amos.

Aliongeza: "Hata hivyo, kila mwezi ulinzi shirikishi wanapita kuchukua fedha za malindo ya mwezi mzima, tunatoa elfu moja kila nyumba, lakini tunashangaa kuona watu wanakabwa na kuibiwa.''

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa ulinzi shirikishi katika eneo hilo, Samson Luhenga, alisema walipokea malalamiko ya wakazi hao na kusema wanashughulikia tatizo hilo na kwa sasa wapo katika jitihada kufanya ulinzi usiku kwa kuzunguka katika maeneo hayo kuhakikisha kuna usalama wa watu na mali zao.

"Ni kweli tumekua tukipokea malalamiko ya watu wanaoibiwa na wengine wanakabwa, lakini nipende kuwahakikishia watu sisi tunafanya kazi na huwa tunapeana zamu," alisema mwenyekiti huyo na kuongeza:

"Kwa hyo tutaangalia endapo watu watalalamika tena kuibiwa, ni nani waliopo kwenye zamu na kwa nini watu wanakabwa ifikapo usiku."

## Gereza latekeleza agizo la Magufuli

**Na Neema Hussein, KATAVI**

GEREZA la Kilimo la Kalilankulukulu wilayani Tanganyika mkoani Katavi, limetekeleza agizo la Rais John Magufuli la kuyataka magereza yote nchini kujitegemee kwa chakula kwa wafungwa na watumishi.

Akisoma taarifa fupi kwa Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, Mkuu wa Gereza, Majuto Masila, alisema gereza hilo limezalisha magunia 1,226 ya mpunga na 605 ya mahindi.

Alisema chakula hicho ambacho kimezalishwa mwaka 2018- 2019 kimewezesha gereza hilo kuondokana na uhaba wa chakula licha ya kuwapo kwa mashamba makubwa ya kulima katika eneo hilo.

Homera alilipongeza gereza hilo kwa kufanya vizuri katika uzalishaji wa chakula na kusema chakula hicho kinatosha hata kulisha magereza mengine.

# Makamishna ardhi wapewa jukumu kodi pango la ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amewaagiza makamishna wasaidizi wa ardhi katika ofisi za mikoa kukaa na taasisi za serikali zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi.

Lengo la kukutana ni kuangalia namna bora ya kulipa madeni wanayodaiwa.

Mabula alitoa agizo hilo jana mkoani Rukwa wakati akizindua ofisi ya ardhi ya mkoa ikiwa ni mfululizo wa uzinduzi wa ofisi za ardhi katika mikoa mbalimbali. Tayari ofisi saba za ardhi katika mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara, Singida, Iringa, Njombe na Songwe zimezinduliwa.

**Bilioni moja ni fedha nyingi sana nawaagiza makamishna wasaidizi wa mikoa kukutana na taasisi pamoja na watu wengine wanaodaiwa kodi ya pango la ardhi.**

Alisema, Mkoa wa Rukwa una taasisi za serikali pamoja na watu binafsi ambao kwa ujumla wao wanadaiwa zaidi ya shilingi bilioni moja kiasi alichokieleza kuwa ni kikubwa na fedha yake ingeweza kutumika katika shughuli za maendeleo kama vile ujenzi wa hospitali au barabara.

Alizitaja baadhi ya taasisi za serikali zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi katika mkoa wa Rukwa ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Chuo Kikuu Huria na kubainisha kuwa katika kumwezesha Rais kufanya kazi ya shughuli za maendeleo kuna wajibu wa kulipa kodi ya pango la ardhi.

"Bilioni moja ni fedha nyingi sana nawaagiza makamishna wasaidizi wa mikoa kukutana na taasisi pamoja na watu wengine wanaodaiwa kodi ya pango la ardhi kukubaliana namna bora ya kulipa fedha wanazodaiwa vinginevyo taratibu za kisheria zitafuata," alisema Mabula.

Kwa mujibu wa Mabula, taasisi za serikali zinatenga fedha kwenye bajeti zake kwa ajili ya kulipia gharama mbalimbali ikiwamo kodi ya pango la ardhi na kutolipa kodi hiyo ni kutotimiza wajibu wa kulipa kodi ya ardhi.

Alisema, wizara yake ilikutana na kampuni na taasisi za serikali zenye malimbikizo makubwa ya kodi ya pango la ardhi mkoani Dodoma na baada ya kukutana ndani ya mwezi mmoja zilikusanywa takriban bilioni ishirini na moja jambo linaonyesha kuwa taasisi hizo zinazo fedha kwa ajili ya kodi hiyo.



Askari wa kikosi cha usalama barabarani, akitoa elimu kwa wananchi na madereva wa vyombo vya moto ya jinsi ya kuvuka kwenye taa za barabarani, zilizowekwa katika barabara kuu ya Mwanza-Tabora, mjini Shinyanga, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Serikali kuandaa rasilimali watu ufundi stadi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema serikali imekusudia kuongeza nguvu zaidi kuandaa rasilimali watu wenye elimu ya ufundi stadi watakaotumika kukamilisha azma ya serikali ya viwanda.



Prof. Ndalichako (pichani) alisema hayo juzi akiwa katika Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma wakati wa uzinduzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Nyamidaho na kueleza serikali imekusudia hadi kufikia mwaka 2025 kujenga vyuo hivyo kila mkoa na kila wilaya.

Alisema kwa mwaka 2019/2020 ujenzi wa vyuo vya VETA katika wilaya 10, umekamilika huku wakiwa wametenga Sh. bilioni 48 na Sh. milioni 637 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika halmashauri 29 ikiwamo ya Uvinza, Kasulu mji na Buhigwe, mkoani Kigoma.

"Vijana wangu hamjapotea kuja VETA niwahakikishie baada ya kumaliza hapa ajira ni nje nje, wapo wenzenu hata kabla hawajamaliza tayari wanakuwa wamepata sehemu za kufanya kazi," alisema.

Awali, akieleza kuanzishwa kwa chuo hicho, Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Dk. Pancras Bujulu, alisema kilianza kujengwa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision na mwaka 2014 kilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na VETA kukabidhiwa Machi 5, 2019.

Baada ya kukabidhiwa walifanya ukarabati na kuongeza baadhi ya majengo ili kikidhi kigezo cha kuwa chuo cha ufundi stadi na mwezi Februari, mwaka huu kilianza kutoa mafunzo ya ufundi kwa fani nne za umeme wa majumbani, ushonaji, uhazili na matumizi ya kompyuta na uashi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kasuli, Simon Anange, aliwataka wanafunzi kuwa waaminifu na kuacha tamaa za kuiba vifaa vya kujifunzia.

## Muda mafunzo kwa vitendo waongezwa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerard Kusaya, amewataka wakuu wa vyuo vya mafunzo ya kilimo nchini kufanya marekebisho ya mitaala 6 ya kufundishia ikiwamo kuongeza muda wa mafunzo kwa vitendo hadi mwaka mmoja kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho ili kuwajengea uzoefu.

Alitoa maagizo hayo jana wakati wa kikao cha pamoja na wakuu wa vyuo vya mafunzo kilimo kujadili namna ya kuboresha mafunzo kwa maofisa ugani ambao wanazalishwa katika vyuo hivyo.

Alisema mitaala inayotumika sasa inaonekana kupitwa na wakati ambapo kumebainika baadhi ya maofisa ugani wanashindwa kuwajibika ipasavyo kwa wakulima wadogo kutokana na kutokuwa na uzoefu wa kutosha.

## SBL yaeleza mchango wake kwa biashara

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya ugonjwa wa corona kuathiri sekta ya utalii, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema imeendelea kutoa mchango mkubwa kwenye mnyororo wa thamani kwa biashara.

Mnyororo huo unajumuisha wakulima, mabaa, wasafirishaji na wasambazaji wa bidhaa zake ambao huajiri maelfu ya watu nchi nzima. Utafiti mdogo uliofanywa na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) mwezi Aprili mwaka huu, ikiwa ni mwezi mmoja baada ya janga la corona kuripotiwa, unaonyesha sekta ya utalii kuwa ndiyo imeathirika vibaya zaidi ambapo mapato yameshuka kwa asilimia 97. Mapato katika sekta ya usafirishaji na uuzaji wa bidhaa mbalimbali yalionekana kuathirika kwa asilimia 70 na 63.

Mkurugenzi wa mahusiano kwa umma wa kampuni hiyo, John Wanyancha, alisema ili kukabiliana na changamoto ya ugonjwa huu, wamekuwa wakiwasaidia washirika wake katika biashara kwa kuwapatia vitakasa mikono, vifaa vya kunawia mikono pamoja na barakoa kwa wafanyakazi wake wa mauzo na kiwandani ili kuwakinga na ugonjwa huo hatari.

Alisema mbali na kusaidia kulinda afya za washirika na wafanyakazi wake dhidi ya corona, kampuni hiyo pia imekuwa ikisaidia juhudi zinazofanywa na serikali kupambana na ugonjwa huo.

Alisema, Machi mwaka huu, ilisaidia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kusambaza vipeperushi vinavyotoa elimu juu ya ugonjwa wa corona kwa wananchi sehemu mbalimbali hapa nchini, na kwamba Aprili pia ilitoa lita 1,250 za vitakasa mkono kwa wizara ikiwa ni mchango wake kusaidia kupambana na janga hilo.

ama
ALHAMISI JULAI 2, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

## Changamoto aina yake wajawazito Shinyanga kuwaacha wakunga jadi



Ukurasa 13

## Mradi Visima Kahama unavyoletea wananchi mbadala nusura ya fisi



Ukurasa 14

## Hofu kupata majibu ya ziada inavyokwamisha upimaji TB

AFYA

# Wadau uzazi mpango wabaini corona inadhibiti utoaji mimba

• Kutoka mazoea hospitali za 'majuu'

**Na Michael Eneza**

NCHI nyingi za ughaibuni na washirika katika nchi zinazoendelea ziko taabani kuhakikisha mpangilio wa kawaida wa kutoa mimba hospitalini unaendelea, baada ya kuvurugwa kuongezeka kasi wagonjwa wa corona.

Taarifa za karibuni za Shirika la Kimataifa la Uzazi wa Mpango (IPPF), zimeainisha kuvurugika sekta ya afya za nchi nyingi duniani, kwa kuelemewa na wagonjwa wa corona.

Inasema mahitaji ya haraka ya kupambana na kuvurugika mifumo ya tiba na kupunguza athari zake, zimejikuta hazina mwitikio wa pamoja wa ushirikiano kutoka nchi mbalimbali.

Mojawapo ni vianzio vya kuporomoka utoaji huduma za kawaida na hasa kwa mahitaji ya uzazi wa mpango, ambazo ni pamoja na kutoa mimba pale mahitaji yanapojitokeza.

Tofauti na mgonjwa kama malaria au hata corona, mtu hawezi kukimbizwa au kufika mwenyewe hospitalini kwa 'ugonjwa' wa mimba, akahitaji kupimwa na kuomba ushauri, au kulipia huduma hiyo, isipokuwa katika baadhi ya mazingira.

Ni hali iliyoleta simanzi, pale wahitaji huduma wanazuiwa ndani na wenza wao. Makundi ya kiharakati ya wanawake na washirika wao, nao wamekuwa wakikipigia kelele kukemea hilo.

Kufanyiwa ukatili wakati watu wanatoka nyumbani kwa shughuli za kawaida, ilikuwa tatizo, sasa wanapokaa hawana fedha, mara nyingi wameelewa na wana 'hasira' ya kuhisi wanadharauliwa. Kukosa pesa ni janga kwa wao ndani ya nyumba.



Kinamama, kundi lililoyumbishwa na corona, sasa kuna upande wa pili, adha za kijinsia. **PICHA: MTANDAO.**

Suala la staha ya maelewano kuhusu uzazi au kutumia utaratibu wa kuhakikisha mimba zinakwepwa, pale mwanamke akiwa hatarini linapuuzwa sababu ya 'presha' tangulizi kifungo cha corona. Ndiyo mimba lazimishi kushamiri.

Wataalamu wa shirika hilo, wanasema magonjwa ya mlipuko kihistoria yanapanua tofauti za kijamii zilizopo, kwa kupunguza upatikanaji huduma muhimu, kwa mfano afya, kwa wanaotegemea mifumo ya kiserikali au umma.

Wanawake wakiwa kundi la waathirika na walio wengi katika ajira na vipato vya uhakika ni wanaume. Ni kwanba, kuna makundi yanayokabiliana na umaskini wa kimaumbile, kutengwa au kubaguliwa.

Mfano hai ni wenye ulemavu, wazee na wasioweza kujitegemea, wakimbizi au wahamiaji na maskini kwa jumla, tabu zao za kupata mahitaji muhimu, ikiwamo tiba au kutoa mimba inazidi.

IPPF inasema hitaji la upatikana vifaa au uhuru wa kutumia njia za uzazi salama kote duniani bado ni tatizo, likitoa makisio kuwa wanawake na mabinti milioni 214 hawatumii vifaa vyovyote kuhakikisha uzazi wa mpango unasimamiwa.

Wengi wanapenda kuzuia mimba, lakini wanakosa uwezo wa kufanya hayo. Hivyo, endapo hesabu ilikuwa ni kabla ya kufumuka janga la corona, wakati wanaume wanatoka kufanya kazi na kwa jumla wanajisikia vizuri, nini kinachojiri wakati wamefungiwa ndani, wana hasira?

Watafiti wa shirika hilo wanasema tofauti za upatikanaji huduma za kuzuia au kutoa mimba zitaongezeka kati ya wanaokaa mijini na waliopo mashambani. Pia, kuna kati ya wanaomudu kufika hospitali binafsi na wanaotegemea za serikali.

Wanawake wasio na fedha za kulipia huduma hizo katika mazingira yanayowazunguka, wanaangukia kubeba jukumu ambalo awali wangelitua kutoka vichwani mwao.

Ugonjwa corona ulipoingia, upatikanaji huduma umedumaa, upatikanaji fedha ukasinyaa vilevile, hali inayoongeza tatizo juu ya jingine, au la tatu.

Imefika mahali wanaharakati wa uzazi wa mpango wenye uhusiano na IPPF, wanazungumzia hali za wanawake wakati wa kufungiwa watu wasitembee kama 'ugaidi wa nyumbani' jinsi wenza wanavyowatesa; hakuna uwezo wa kuzuia hali hiyo kisheria.

Wakilinganisha uwezo wa wanawake kupata huduma hiyo kabla ya janga la corona, wataalamu hao wanasema theluthi moja walikuwa hawaimudu, kwani kupata dawa za kutumia kwa siku mbili ilikuwa inagharimu Dola za Marekani (wastani Sh. milioni 10) na kwa upasuaji dola 350 ( Sh. 770,000).

Hata hivyo hospitali za umma kwa jumla hakutoa huduma hizo na binafsi zinakuwa zimeelemewa, hali inayovurugwa zaidi na janga la corona.

Mimba zisizotakiwa zinaongezeka, kutokana na ushirikiano kupungua kati ya wenza na huduma hospitalini kuelemewa na corona. Watu wanapata ushauri nje ya hospitali, kwani hawawezi kupata huduma hiyo huko.

AFYA

# Changamoto aina yake wajawazito Shinyanga kuwaacha wakunga jadi

- Mkoa watunga sheria za kuwabana
- Wafuatiliwa hadi waliko kona zote



Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, mkoa wa Sinyanga, Azza Hamadi, akitoa misaada ya vifaa vya uzazi katika Zahanati ya Bunonga, mkoani Shinyanga. Nyingine ndogo, akizungumza na kinamama katika tukio hilo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MKOA Shinyanga unakabiliwa na vifo vingi vitokanavyo na uzazi, sababu kuu ni wajawazito kuendekeza mila zilizopitwa na wakati, hawahudhurii kliniki na kuna matukio ya kujifungulia majumbani au kwa wakunga wa jadi.

Katika kulikabili hilo, mwaka jana mkoa ulipanga mkakati kupunguza tatizo kwa kutunga sheria ndogo zinazowabana wajawazito wakajifungue kwenye huduma rasmi za afya kwa lazima.

Ni sheria inayofika ngazi ya kijiji, ikiwaorodhesha wajawazito kwenye maeneo husika na kisha mahudhirio yao kliniki yanafuatiliwa kuhakikisha wanajifungua hospitalini na watakaokiuka hayo, watatozwa faini ya Sh. 20, 000.

Wasimamizi wakuu wa sheria hizo, ni wenyeviti wa vijiji, wanaoaminika kuwa karibu na wananchi na wazifahamu kaya, hata kuweza kuhoji kupitia ofisi za kijiji, pale watakapoona walakini.

**MRATIBU UZAZI**

Mratibu wa Huduma ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, mkoa wa Shinyanga, Joyce Kondolo, anasema kutungwa sheria hizo kwa sasa umefikia ngazi ya halmashauri na baadae itapelekwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, kutafuta kuidhinishwa rasmi.

Anasema, wakati wakisubiri sheria hiyo ianze kazi, pia wanatoa elimu kwa wajawazito kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema na mhusika anajifungua penye huduma za afya.

> **“ Mratibu wa Huduma ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, mkoa wa Shinyanga, Joyce Kondolo, anasema kutungwa sheria hizo kwa sasa umefikia ngazi ya halmashauri na baadae itapelekwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, kutafuta kuidhinishwa rasmi.**

“Utamaduni za watu wa Shinyanga, wanapenda kujifungulia watoto majumbani, pamoja na kwa wakunga wa jadi,” anasema na inaendelea:

“Pale wanapozidiwa, ndipo hukimbilia hospitali ambayo wengine wanakuwa katika hali mbaya aidha kwa umwagaji damu nyingi na hatimaye kusababisha kifo.”

Kondolo anasema, kwa miaka minne mfululizo tangu mwaka 2015 hadi 2019, walitoa elimu kubwa kwa wajawazito na wakunga wa jadi kuhusu umuhimu wa kujifungua penye huduma za afya, hata kupunguza vifo vya mama na mtoto zitokanavyo na uzazi.

Mratibu huyo anataja takwimu zilizopo kimkoa kwa miaka na idadi katika mabano:Shinyanga 2015-2019 (60); 2016 (74); 2017 (73); 2018 (56), huku mwaka 2019 vimepungua hadi vifo 50.

Anasema, matarajio ya mwaka huu, 2020, takwimu zake zitatolewa mwezi Desemba.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, matumizi ya dawa za kienyeji kuongeza uchungu, imekuwa na kawaida ya kuwazidi na hatimaye inapasua kizazi chao, hata kusababisha kifo cha mtoto.

Lingine analitaja, ni mama kujifungua watoto wengi bila kuachiana nafasi, hali inayokifanya kizazi kulegea na wakati wa kujifungua wanamwaga damu nyingi, hata kupoteza maisha.

**RC ACHANGIA**

Zainab Telack, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anasema sheria inapaswa kwenda sambamba ya uhalisia wa maisha ya jamiii, elimu ikipaswa kuendelea kutolewa na wahusika wahudhurie kliniki na kujifungua hospitalini.

“Mkoa una jumla ya vituo vya kutoa huduma za afya 240, zahanati 206, vituo vya afya 23 na hospitali nane (hospitali tano za serikali; moja ya taasisi ya dini na mbili za binafsi) na kliniki tano,” anasema Zainab.

“Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 mkoa pia tulipokea kiasi cha Sh.milioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mbili katika Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na ujenzi wa hospitali hizo umekamilika,

Mkuu wa Mkoa anasema, lengo ni kuviwezesha vituo husika kutoa huduma za upasuaji dharura kwa kinamama wajawazito na ujenzi wa vituo vya afya vyote tisa umekamilika kwa asilimia 100 na baadhi ya majengo yameanza kutumika kwa huduma hiyo.

Anasisitiza, wajawazito watumie huduma hizo za afya zilizoandaliwa na serikali wakajifungue, ili kusaidia kupunguza madhara ya vifo vya mama na mtoto kitaifa.

**MKUNGA JADI**

Salome Dotto, ni mkunga wa jadi aliyeacha kutoka kijiji cha Bunonga Mwamala, wilayani Shinyanga, anasema hivi sasa vifo vya mama na mtoto vimepungua kwa kiasi kikubwa, tofauti na zamani.

Anakiri wakunga wa jadi na jami walishapigwa marufuku uzalishaji wajawazito na wanachokifanya sasa, ni kuwapatia elimu ya kuhudhuria kliniki mapema, pamoja na kuwasindikiza kujifungua hospitalini.

“Wakunga wa jadi sasa hivi tunafanya kazi na serikali ya kutoa elimu kwa wajawazito ndani ya jamii, juu ya umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema na kujifungua watoto hospitalini.

“Pia, tuna daftari la orodha ya wajawazito wote na huwa tunafuatilia taarifa zao lengo ni kuhakikisha wanajifungua salama,” anasema.

**MBUNGE AJITOA**

Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Sinyanga, Azza Hamadi, anaeleza kuguswa na vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi na anaamua kutafuta msaada wa vitanda vya uzazi na vifaa tiba, kutoka ubalozi wa China, ili kupunguza vifo hivyo.

Anasema, wajawazito wanapata tabu wakati wa kujifungua na katika baadhi ya hospitali, kuna upungufu wa vitanda vya kisasa kwa wajawazito na ndio maana aliguswa na kutafuta ufadhili huo kugawa kwenye zahanati na vituo vya afya mkoa mzima.

“Kinamama wanapata adha kubwa wanapohitaji huduma za afya. Baada ya kuona jinsi kinamama hawa wanavyoteseka, niliamua kuanza kutafuta watu wa kutusaidia.

“Nashukuru ubalozi wa China nchini Tanzania kukubali kunipatia vifaa hivi, kwa ajili ya kupunguza vifo vya mama na mtoto,” anafafanua mbunge huyo.

Kwa mujibu wa Mbunge Azza, jumla ya msaada wake unajumuisha vitanda vya kujifungua, mashuka, mashine za kupima damu, sukari, joto, mapigo ya moyo, pamoja na vifaa vinavyotumika katika chumba cha kujifungulia.

**MJAMZITO ASIMULIA**

Ester (jina la pili tunalo), ni mjamzito na mkazi wa mjini Shinyanga, anasimulia uzao wake wa kwanza alijifungua kwenye huduma za kiafya mahali pasipo salama na alipata huduma nzuri, licha ya uchungu kumgomea, alipewa huduma na alijifungua salama.

Anasema, hivi sasa amekuwa akihudhuria kliniki kwa wakati kujua maendeleo ya mtoto tumboni na mengine ya kiafya, lengo ni kujifungua salama.

“Natoa wito kwa wajawazito wenzangu ambao wapo majumbani wahudhurie kliniki mapema, ili wapimwe na kupatiwa maendeleo ya mtoto tumboni, siku zikifika waje hospitali kujifungua sehemu ambayo ni salama, kuliko nyumbani,” anashauri.

Anahitimisha kuwa vifo vya uzazi vitapungua mkoani Shinyanga kupitia elimu sahihi inayopaswa kutolewa hata vijijini, huku kukichukuliwa hatua kwa wajawazito wanaopuuzia kanuni sahihi, ikiwamo kupitia majumbani wanakopatikana wakunga wa jadi.

MAZINGIRA

# Mradi Visima Kahama unavyoletea wananchi mbadala nusura ya fisi

## • Safari Km. 18 alfajiri sasa hadithi



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akikagua mabomba ya maji yatakayotumika kusambaza majisafi katika Kata ya Ngogwa. Nyuma yake, Meneja wa SHUWASA, Flaviana Kifizo.

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

NGOGWA imo katika kata 20 zinazounda Halmashauri ya Mji wa Kahama, mkoani Shinyanga. Iko pembezoni kwa zaidi ya kilometa tatu na imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji huduma wa majisafi na salama kwa kipindi kirefu.

Inakadiriwa wakazi wake ni 10,350 kwa kwa marejeo ya Sensa ya Watu na Makazi kitaifa. Panadaiwa kusumbuliwa na adha za uvamizi wa fisi, wanapoamka alfajiri kuelekea kutafuta huduma ya maji kata jirani, umbali wa kilometa 18, panakozungukwa na milima, huku uhusiano wa kifamilia nao ukiingia utata.

Kati ya mwaka 1996 hadi 1997, kata hiyo ilitawaliwa na ukame na hata kulazimika kununua maji yanayotolewa mjini Kahama, ndoo moja inanunuliwa Sh. 1,000 na wakazi husika wanashindwa kumudu gharama, hali inayowafanya baadhi wahamie kata jirani.

**MRADI VISIMA**

Mwaka 1998, wakazi husika walichukua hatua kuchimba visima vifupi, ambavyo hata hivyo, maji yake hayakuwa safi na salama.

Hata hivyo, visima hivyo vilikauka kutokana na kutumiwa na wananchi na mifugo. Mwaka 1999 hadi 2000, kuliibuka tena janga la ukame na kupoteza mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Pia, katika mwaka wa kilimo 2018/19, kata ilikumbwa na ukame uliowasababishia wananchi hasara kubwa shambani, ilipokausha mazao na wafugaji kufilisika kwa mifugo kufa na wanafunzi badala ya kusoma, walitumia muda kutafuta maji katika kata za jirani.

Diwani wa Kata, Kamuri Mayunga, alilifikisha hilo katika vikao vya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Kahama, kudai upatikane mradi wa kuchimba kisima kirefu cha kuhudumia vijiji vitano.

Mayunga anasema, ukame katika kata hiyo lilisababisha baadhi ya wananchi kukimbilia kata jirani, kwa sababu ya ukosefu wa maji na kuathiri shughuli za kimaendeleo, hasa uzalishaji mali.

Anasema, wanafunzi walishindwa kwenda shule vyema kusoma na badala yake walitumiwa na wazazi kwenda kutafuta huduma ya maji kata ya Busoka, zaidi ya kilometa 18 kwenda na kurudi na wengi kuacha masomo kabisa.

Inaelezwa, mabomba ya maji ya kata hayakutoa huduma ya maji na ukawepo uzoefu, kila mwezi wa saba walikumbwa na janga ukame, wengi wakachukua jukumu la kuihama kata.

**WANANCHI KATA**

Mary John, mkazi kijiji cha Ngogwa anasema kati ya mwaka 2012 hadi 2019, kijiji kilipata ukame na akalazimika kutembea umbali kilomita 18 kwenda kata ya Busoka kuchota maji na kuna wakati walilazimika kununua maji ndoo moja kwa Sh. 1000.

Anasimulia kwamba, waliamka alfajiri kwa safari ya kutafuta majisafi na salama katika kata ya Busoka, walikokumbwa na mikasa ya kuvamiwa na fisi, kutokana na kata kuzungukwa na milima na mapango ambayo ni makazi ya fisi.

Mama huyo anasifu mradi umewasaidia kinamama kushambuliwa na adha ya kudhuriwa na wanyama, kisima kipya kirefu kinachohudumia vijiji vyote, ingawa bado havitoshelezi mahitaji.



Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Shinyanga (SHUWASA), Flaviana Kifizo, katika mradi wa ujenzi wa tanki la maji lililopo Kahama. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**FISI VANAVYOVAMIA**

Mkazi, Peter Edward, anasema fisi wamekuwa wakiwavamia wananchi katika nyendo zao za kutafuta maji, huku mbadala shughuli za maendeleo zikizisuasua na miezi mitatu ambayo wanafunzi walikuwa nyumbani (shule imefunguliwa Jumatatu iliyopita), wazazi waliwatuma kutafuta maji, badala ya kuwacha kujisomea.

"Tulikuwa tunavamiwa na fisi wakati tukiwasindikiza wake zetu kwenda kuchota maji. Sasa tunavamiwa saa 24, mchana na usiku na hivi karibuni moja ya familia ilivamiwa mchana na fisi na kushambuliwa ng'ombe na mbuzi.

"Wanyama hao sio wa kutafuta, wanaonekana wakati wote na tunaziomba mamlaka zinazohusika na kupambana na wanyama hawa, kuja kuwadhibiti ili wasiendelee kuvamia wananchi hasa wanafunzi," anaeleza Mary.

Anasema, wanyama hao wanazidi kuongezeka kutokana na kuwepo chakula chao, mbuzi, kondoo na ng'ombe, baadhi wanajificha kwenye mapango yanayozunguka kata na usiku wanatoka kuvamia makazi.

Celina Paulo, kutoka kijiji cha Nyamela, anasema fisi ni kikwazo kwao kwaenda kuchota maji asubuhi na anaelekeza ombi serikalini kuhakikisha adha ya wanyama wavamizi wanaodolewa, kuwaacha wawe salama.

**DC/ BOSIN SHUWASA**

Flaviana Kifizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya MajiSafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), anasema kutokana na changamoto hiyo, serikali imeanza kujenga mradi mkubwa wa maji, kwa wana - kata ya Ngogwa na Kitwana, wenye thamani ya Sh. bilioni 2.4

Anasema sasa umeshakamilika kwa asilimia 95 na kwa matarajio kumalizika mwezi ujao na kuanza kunufaisha zaidi ya wakazi 1000 wanaoishi pembezoni mwa Halmashauri ya Mji wa Kahama.

"Ujenzi wa matanki mawili ya Ngogwa na Kitwana, umekamilika na kwa sasa, tunatarajia kuanza kulaza mabomba, ili kuruhusu maji kuanza kutumiwa na wananchi.

"Pia, tutajenga vituo 13 vya kuchota maji, ambayo yatawawezesha wananchi kupata huduma za maji safi na salama na itakuwa suluhisho la kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo," anafafanua Kifizi.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, anawataka wananchi wa kata za Ngogwa na Kitwana wasiweke vikwazo pindi itakapoanza hatua ya kuchimbwa mitaro ya kupitisha mabomba ya maji, kwani hakuna wa kulipwa fidia.

Macha anawaagiza wahusika wa Idara ya Wanyamapori, kudhibiti madhara kwa wananchi, ili kuwapatia wanya wananchi kuendelea na shughuli za uzalishaji mali, hasa kwenye kilimo chenye tija na ufugaji.

AFYA

## WANAHARAKATI MUKIKUTE

# Hofu kupata majibu ya ziada inavyokwamisha upimaji TB

## • Walengwa shaka yao HIV, corona

**Na Sabato Kasika**



Watoa huduma wa klabu za kifua kifuu za Mukikute, wakiingia nyumbani kwa mmoja wa wakazi wa Mbagala Kiburugwa, Dar es Salaam, kutoa elimu.

Ni kampeni ya nyumba kwa nyumba kutoa elimu na kuhamasisha jamii kupima ugonjwa wa kifua kikuu, wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, sasa zimefikia watu 6808.

Waendeshaji kampeni ni vilabu vya maradhi ya kifua kikuu, chini ya Shirika la Mapambano ya Kifua Kikuu na Ukimwi Temeke (Mukikute), lililopo Temeke, ikifanya kazi kwa ubia wa karibu na Halmashauri ya Wilaya Temeke.

Makamu Mwenyekiti wa Mukikute, Seif Mchila, anasema nyendo zao karibuni zimekuwa ikionishwa na Maadhimisho ya Siku ya Dawa za Kulevya, yaliyoanza tarehe 15 hadi kilele 26, mwezi uliopita.

Mchila anasema, utekelezaji wao wanashirikiana kwa karibu na Idara za Kifua Kikuu na Ukoma, Afya ya Akili na Dawa za Kulevya ya Manispaa ya Temeke, kuwaibua wangojwa wa kifua kikuu wa wilaya Temeke.

" Huwa wanapata huduma ya dawa katika zahanati zote za manispaa na wataalamu wa afya wa manispaa, hutoa mafunzo kwa wanachama wetu ya jinsi ya kuhudumia wagonjwa wa kifua kikuu," anasema.

Ili kunusuru jamii na janga la kifua kikuu, wabia hao wamekuwa wakiwaelekeza watoa huduma wa Mukikute, kuwapelekea dawa wagonjwa walio mbali na zahanati

"Unajua siyo sisi tu tunaoibua wagonjwa, bali wapo wanaokwenda hospitali wenyewe na kama watakuwa wanaishi mbali na zahanati, watoa huduma wa Mukikute hupewa jukumu kuwapelekea dawa nyumbani," anasema.

**CHANGAMOTO**

Mchila ana ushuhuda wa changamoto, baadhi ya wanaojitokeza katika tukio hilo ni waoga na wanahusisha na uwezekano wa kugundua maradhi mengine.

Anasema, inachangiwa na uchache wa waliojitokeza kupima afya ya kifua kikuu, ingawa idadi ya waliofikwa na kupata elimu ni kubwa.

Ni elimu iliyotolewa na wahamasishaji kutoka klabu za TB ambazo ziko chini ya shirika la Mapambano ya Kifua Kikuu na Ukimwi Temeke (Mukikute), yenye maskani eneo la Temeke .

"Kata hizo ni Azimio, Kiburugwa na Keko, lakini idadi ya waliojitokeza kupima kujua kama wana maambukizi ya kifua kikuu 166 tu, kati ya watu 6808 waliofikiwa na klabu zetu za TB," anasema Mchila.

Anasema, watu 130 katika Kata ya Keko walipimwa na 10 ndio waligundulika kuumwa; kata ya Azimio kuna watu 15 waliopimwa, saba kati yao wakigundulika kuwa na kifua kikuu.

> **Klabu zetu zimefanya kazi kubwa kwenye kampeni hizo, lakini hofu hiyo," anasema, akieleza kuwa inaonyesha bado kuna haja ya elimu zaidi kwenye jamii, kutambua vyanzo vya ugonjwa huo na kuuepuka, kuliko kuogopa kupima afya.**

"Kwa upande wa Kata ya Kiburugwa walijitokeza watu 21 walioopima afya zao na wawili kati waligundulika kuwa na TB, wote hao kutoka katika kata hizo wameshaanza kutumia dawa," anasema.

**KWA NINI HAWAPIME?**

Mdau huyo wa afya ya umma, anasema sababu kubwa ya kutopima afya, ni hofu kwamba ama wangezuiwa kwenye kambi za wagonjwa wa corona au kupimwa virusi vya Ukimwi.

"Klabu zetu zimefanya kazi kubwa kwenye kampeni hizo, lakini hofu hiyo," anasema, akieleza kuwa inaonyesha bado kuna haja ya elimu zaidi kwenye jamii, kutambua vyanzo vya ugonjwa huo na kuuepuka, kuliko kuogopa kupima afya.

"Haikuhusiana na mambo ya corona au Ukimwi, ingawa dalili za maambukizi ya kifua kikuu zinafanana na Ukimwi," anasema.

Mchila anasema, licha ya wahamasishaji wa klabu kujitahidi kufafanua, baadhi ya watu waliofikiwa walisita kuafiki, wakisisitiza wanahofia ama kuwekwa karantini au kupimwa Ukimwi.

Anasema, walengwa wa kampeni walikuwa watu wa rika zote, wakiwamo wanaopatikana katika vilabu vya pombe za kienyeji, watumiaji dawa za kulevya na walioko kwenye 'mageto'.

Pia, anasema kuna shida zilizo juu ya uwezo wao na jamii kwa ujumla, kama vile kukosa fedha za kuchangia vipimo, mtu anapohisi ugonjwa, lakini akapima makohozi na hakukutwa na athari yoyote.

"Yaani ni kwamba, iwapo TB haitaonekana katika makohozi, mgonjwa analazimika kupiga X-ray ambayo anatatakiwa angalau kuchangia gharama kidogo ya Sh. 15,000, lakini mtu hana," anasema.

Anashauri uwezekano wa kutolewa huduma zote kwa wagonjwa wa TB bure, hasa watu wa hali ya chini, ambao Mukikute imewatembelea baadhi yao na kuwapa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

**KIFUA KIKUU?**

Dk. Emmanuel James, kutoka Kitengo cha Kifua Kikuu, katika Zahanati ya Tambukareli, iliyoko Kata ya Azimio, anasema ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea aina ya bakteria visivyoonekana kwa macho ya kawaida, bali darubini.

"Kuna aina mbili za kifua kikuu kinachoshambulia mapafu na nje ya mapafu kama mifupa. Lakini ikumbukwe kwamba, kifua kikuu cha mapafu ndiyo chanzo cha maambukizi," anasema Dk. James.

Anasema namna mtu anavyoambukizwa ni kwa njia ya hewa kutoka kwa mwenye ugonjwa ambaye hajaanza matibabu.

"Vimelea hivyo husambaa kwenye hewa na iwapo kuna mtu mwingine ambaye hana ugonjwa huo, akivuta hewa hiyo anaweza kuambukizwa kirahisi, hivyo ni vyema watu kupima afya zao," anasema.

Dk. James anasema, katika zahanati hiyo, kati ya Januari hadi Machi mwaka jana, watu 71 walijitokeza kupima afya dhidi ya kifua kikuu, lakini kwa mwaka huu katika kipindi kama hicho kuna mahudhurio ya watu 66.

"Nimejaribu kutoa mfano huo mdogo, lakini ukweli ni kwamba elimu zaidi inahitajika kwa jamii, ili kutambua umuhimu wa kupima afya, pia kuzingatia ratiba ya matumizi ya dawa za kifua kikuu," anasema.

Dk. James anasema katika zahanati ya Tambukareli, wagonjwa wanaoibuliwa na klabu ya TB ya eneo hilo, wanaogunduliwa hufika kupata dawa.

Anasema, si kila anayeumwa kifua kikuu ana VVU, hali kadhalika si kila anayeishi na VVU ana kifua kikuu, ila kwa kanuni kila anayehisiwa anao anashauriwa kupima na akikutwa nayo, ataanzishiwa dawa za kupunguza makali ya VVU na zinazozuia magonjwa nyemelezi.

"Kwa ujumla ni kwamba, kifua kikuu kinatibika pale mgonjwa anapozingatia maelekezo na taratibu za matibabu na hasa ratiba ya kunywa dawa, ambayo baadhi ya wagonjwa wamekuwa hawazingatii," anasema.

Anafafanua dawa hizo hutolewa kwa utaratibu maaluma wa umezaji kila siku, kwa usimamisi wa mtaalamu afya au mwanajamii aliyepata mafunzo.



Mwenyekiti wa Klabu ya Kifua Kikuu Keko, Loi Muyeya (kulia), akimpa dawa za ugonjwa huo mhusika mmoja. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**



# Bunge lajivunia Tanzania kutoitwa 'shamba la bibi'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge Job Ndugai, amesema Bunge la 11 linajivunia kuiondoa Tanzania kuwa shamba la bibi kwa kutunga sheria za kuwamilikisha rasilimali zao ikiwamo madini ili Watanzania wanufaike nazo.

Julai 2017, Bunge hilo lilitunga sheria mbili muhimu za uchimbaji madini ambazo zina lengo la kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya madini ili wananchi wanufaike na maliasili nchini.

Kauli hiyo aliitoa juzi ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Mabunge Duniani ambayo huadhimishwa Juni 30 kila mwaka. Ndugai alisema Bunge la Tanzania limetoa mchango mkubwa wa kimaendeleo ikiwamo kutungwa kwa sheria hizo ili Watanzania wanufaike na rasilimali zao za asili ikiwamo madini badala ya kunufaisha wageni.

**Tulijisikia faraja sana kufanya jambo hilo kwasababu Watanzania wengi wamepiga kelele miaka mingi kwamba sisi ni shamba la bibi, sheria imeondoa Tanzania kuwa shamba la bibi.**

"Bunge la 11 tunajivunia mengi, lakini katika jambo ambalo mimi naliweka namba moja ni pale tulipoafikiana na serikali yetu kutunga sheria ambazo zinawamilikisha Watanzania rasilimali zao za asili ikiwamo madini yetu," alisema.

"Tulijisikia faraja sana kufanya jambo hilo kwasababu Watanzania wengi wamepiga kelele miaka mingi kwamba sisi ni shamba la bibi, sheria imeondoa Tanzania kuwa shamba la bibi."

Alisema pia ilitunga sheria inayoendana na masuala hayo ambayo ilitoa nafasi kwa serikali kuangalia mikataba yote ya zamani ambayo ilikuwa imeingiwa na serikali zilizopita ili iangaliwe na ambayo haina maslahi kwa Taifa ifumuliwe na kuandikwa upya.

Akizungumzia jambo ambalo hatalisahau, Spika Ndugai alisema kitu ambacho hatakisahau ni kufanya kazi katikati ya uwapo wa ugonjwa wa corona.

"Ulikuwa mtihani mkubwa kwa Bunge letu kiasi ambacho ilibidi mambo mengi sana ya kufanya kazi ndani ya Bunge, mifumo ya uendeshaji kubadilika ili kuendana na hali husika na kuwakinga na ugonjwa wa corona wabunge, wananchi na watumishi wengine wa serikali waliokuja bungeni," alisema.

Alisema mambo mengi yalirekebishwa ya uendeshaji wa Bunge.

Hivi karibuni akiwasilisha bajeti ya Wizara ya Madini, Dotto Biteko, alisema uwapo wa sheria mpya za madini zimechangia kuongezeka kwa makusanyo kwenye sekta hiyo kutoka Sh. bilioni 194 kwa mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. bilioni 470 kwa mwaka 2019/20.



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu (kushoto), akiongoza dua ya kuliombea taifa na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), uliofanyika jijini Dodoma juzi. Wapili kushoto ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watanzania waishio Marekani wamsifu JPM ushindi dhidi corona

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

JUMUIYA ya Watanzania wanaoishi nchini Marekani, (ATC), imempongeza Rais John Magufuli alivyofanikisha mapambano ya ugonjwa corona nchini.

Pongezi hiyo zilitolewa na Mwakilishi wa Watanzania hao, Kapteni Amos Lwiza, alipokuwa akikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vya kujikinga na ugonjwa huo kwa ajili ya zahanati na vituo vya afya Wilaya ya Chamwino wenye thamani ya Sh. milioni 7.4.

Akizungumza jana wakati wa makabidhiano ya msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, Kapteni Lwiza, alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya corona.

Kapteni Lwiza, alisema Watanzania wanaoishi nchini Marekani, katika Majimbo ya Washington DC, Maryland na Virginia (DMV), wanajiona fahari kwa namna Rais Magufuli, alivyofanikisha ushindi dhidi ya mapambano ya virusi vya corona nchini.

"Sisi kama Watanzania tunaona fahari kubwa sana kwetu na tunatembea kifua mbele hivi sasa kutokana na rais, alivyofanikisha mapambano haya ya corona na tumeamua kumuunga mkono katika juhudi hizo kwa kutoa msaada huu wa vifaa vya kujikinga na corona," alisema.

Alisema vifaa walivyotoa ni sabuni, vitakasa mikono pamoja na grovu ambazo zitasambazwa katika zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali zilizopo wilayani Chamwino.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya hiyo, Nyamoga, alishukuru kwa msaada huo ambao utasaidia kuendeleza mapambano ya corona.

"Corona bado ipo hivyo hatuna budi kuendelea kuchukua tahadhari zote zinazotolewa na Wizara ya Afya, hivyo kwa kupata vifaa hivi tutahakikisha kuwa tunavipeleka katika maeneo yote yenye uhitaji," alisema Nyamoga.

Alitoa wito kwa wadau kujitokeza kutoa misaada kutokana na mahitaji kuwa juu baada ya shule kufunguliwa.

# Mavunde aomba viongozi wa dini kuombea uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amewaomba viongozi wa dini nchini kuliombea taifa, hasa wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba, 2020 ili ufanyike kwa amani na utulivu.

Mavunde, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa uchaguzi wa Baraza Kuu la Waislamu Mkoa wa Dodoma (BAKWATA).

Alisema viongozi wa dini nchini, wanatakiwa kuendelea kuliombea Taifa pamoja na uchaguzi mkuu, mwaka huu, ili ufanyike kwa amani na utulivu.

"Viongozi wa dini mnalojukumu la kuendelea kuliombea taifa letu, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu 2020, ili liweze kupita kwa salama," alisema Mavunde.

Pia, alisema serikali ya awamu ya tano imefanya mambo makubwa na kwamba viongozi hao hawana budi kuendelea kumwombea awe na afya njema Rais John Magufuli ili ashinde awamu ya pili ya uongozi wake na kumalizia kazi aliyoanza kuifanya.

Alilipongeza baraza hilo kwa kufanya mkutano wake kwa mujibu wa Katiba tofauti na taasisi nyingine.

"Niwapongeze BAKWATA, nyinyi mmefanya mkutano wenu wa uchaguzi ili kuwachagua viongozi kwa mujibu wa Katiba yenu tofauti na taasisi nyingine kufanya uchaguzi hadi wavutane kwanza," alisema Mavunde.

Awali, Katibu wa BAKWATA, Mkoa wa Dodoma, Hussein Kuzungu, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo usafiri na kompyuta, kwa ajili ya kutekeleza majukumu.

"Lakini katika kipindi cha miaka mitano BAKWATA tumeweza kurejesha mali zetu pamoja na msikiti wa barabara ya tisa uliokuwa umuhodhiwa na wavamizi, na tunamshukuru mkuu wa mkoa pamoja na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma kwa kutusaidia katika hili," alifafanua Kuzungu.

Kwa upande wake, Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Shabani, alisema viongozi wa dini hawana budi kumuunga mkono Rais Magufuli, kutokana na kuwathamini tofauti na hapo awali.

"Katika kipindi hichi cha Magufuli, viongozi wa dini tumeheshimika sana amekuwa akituamini sana na kututumia katika mambo mbalimbali, leo hii kiongozi wa dini akienda katika ofisi ya umma anahudumiwa haraka sana kuliko hata kiongozi wa CCM," alisema.

Aliwaasa Watanzania kuthamini utendaji kazi wa Rais Magufuli, kwa kuwa hata mataifa ya jirani yanatamani kumpata mtu kama yeye.

"Kupatikana kwa rais huyu ni maombi yetu ambayo tulikuwa tukiyaomba kipindi cha nyuma na Mungu katujibu kwa kutupa Magufuli, hivyo lazima tumthamini kwani mataifa mengine yanatamani hata kuwa na mtu kama yeye," alifafanua.



HABARI MBEYA

# Mwili wafukuliwa siku 90 baada kuzikwa

Na Grace Mwakalinga, MBARALI

MWILI wa marehemu Tulizo Konga (38), ambaye tangu azikwe siku 90 zilizopita katika kijiji cha Igumbilo wilayani Mbarali, umefukuliwa kufanyiwa uchunguzi ili kubaini chanzo cha kifo chake kutokana na utata uliokuwapo.

Zoezi la kufukua mwili huo lilifanyika jana baada ya kupata kibali kutoka mahakama na kusimamiwa na Jeshi la Polisi pamoja na jopo la madaktari wawili akiwamo wa familia na serikali.

Sababu za kufukuliwa mwili huo zilitokana na ndugu wa marehemu kuingiwa na mashaka baada ya kupata taarifa za msiba kutoka kwa majirani badala ya mume wake, Kelvin Mwanjemba.

Msemaji wa familia ya marehemu Msafiri Mlowezi, alisema kifo cha ndugu yao kiligubikwa na utata kutokana na familia ya mume wa marehemu kutotoa taarifa za kuumwa wala kifo badala yake walizisikia kwa majirani.

**Kifo cha ndugu yao kiligubikwa na utata kutokana na familia ya mume wa marehemu kutotoa taarifa za kuumwa wala kifo badala yake walizisikia kwa majirani.**

Pia, alisema baada ya kufanyika taratibu zote za mazishi kutoka kwa mume wa marehemu, ndugu wa Tulizo walizuiliwa kuuaga mwili hadi ulipozikwa kwenye makaburi ya Igumbilo.

Kutokana na mazingira hayo familia ya Konga ilikata rufani kwenye vyombo vya sheria ikiomba haki itendeke na kubaini ukweli endapo ndugu yao alikufa kifo cha kawaida.

Msemaji wa familia hiyo, Mlowezi alisema walifikisha malalamiko hayo kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, wakiomba mwili wa ndugu yao ufukuliwe ili wahakikishe kama yeye na hakuna majeraha yoyote yaliyochangia kuondoa uhai wake.

"Familia ya Konga tulishikamana sana kuhakikisha ukweli juu ya kifo cha ndugu yetu unabainika kwa sababu alikufa ghafla hakuna taarifa za kuumwa na tulipofuatilia kwenye hospitali ya Chimala, daktari alituambia alimpokea Tulizo akiwa amepoteza maisha na sio akiwa mgonjwa kama mume wake anavyodai sambamba na hilo sisi hatukuruhisiwa kabisa kufunua jeneza la marehemu ili tumuage hivyo mazingira hayo yalitupa maswali mengi," alisema Mlowezi.

Baada ya zoezi la ufukuaji na baadhi ya ndugu kumwangalia marehemu wakiwa eneo la makaburi ya Igumbilo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na madaktari waliupekea mwili kwenye Hospitali ya Chimali kwa ajili ya uchunguzi zaidi kubaini chanzo cha kifo chake.

Baba wa marehemu, Ashery Konga, alilipongeza Jeshi la Polisi na madaktari kukubali kuufukua mwili wa mwanawe, kumuangalia na kumfanyia uchunguzi na kusisitiza endapo watabaini majeraha au kiungo chochote hakipo kwenye mwili wake sheria ichukue mkondo wake, huku akiliomba Jeshi la Polisi kuweka ulinzi kwa familia yao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Igumbilo, Steven Mwakapetela, aliwaomba ndugu wa marehemu kuendelea kuwa watulivu wakati vyombo vya sheria vikiendelea na uchunguzi wa sababu ya kifo cha mpendwa wao.

Tulizo alifariki dunia Machi 25, mwaka huu akiwa nyumbani kwake na mumewe Mwanjemba na kuzikwa Machi 28.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei kwa sasa wanasubiri taarifa kutoka kwa madaktari kubaini chanzo cha kifo, huku akifafanua kuwa historia ya marehemu inaonyesha kulikuwa na uvimbe kichwani uliosababisha ugonjwa wa kifafa ambao huenda ulimsababishia kifo.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Highland Estate, inayojihusisha na kilimo cha zao la mpunga na mazao mengine pamoja ufugaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakiendelea na zoezi la ukoboaji wa zao hilo, kwa kutumia mashine kubwa na ya kisasa, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## DC ahamasisha vijana kuchangamkia fursa

Na Grace Mwakalinga, CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi, amewahamasisha vijana kuendelea kuzitumia vyema fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko kwenye mazingira yao ili ziwasaidie kujiingizia kipato.

Mahundi alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu hamasa waliyonayo kuzichangamkia fursa za kiuchumi kwenye maeneo yanayowazunguka.

Alisema kuna fursa nyingi kwenye jamii, lakini shida iliyopo ni vijana kupenda kutafuniwa kila kitu na baadaye kuishia kulalamikia serikali kwamba haiwasaidii wakati wanayo nafasi ya kuanzisha vikundi vya ujasiriamali na kupata mikopo kutoka kwenye halmashauri.

"Mimi ni kijana nafahamu ni wapi tunakwama, wako walioamaliza elimu ya juu tangu mwaka 2015, lakini hadi sasa wako nyumbani kwao hawana shughuli yoyote ya kufanya ya kuwaingizia kipato, cha muhimu kwao ni kushinda kwenye vijiwe na wanawake kujiremba kuiba waume za watu, hawajui wanachelewesha maendeleo yao," alisema Mahundi.

Aliwakaribisha vijana kutoka maeneo mbalimbali nchini kuwekeza kwenye sekta ya uchimbaji na ununuzi wa madini ya dhahabu ambayo kwa kiasi kikubwa yameinua uchumi wa Wilaya ya Chunya. Alisema biashara ya madini ina faida kubwa, hivyo kijana akiwekeza nguvu kazi yake na mtaji anaweza kupata faida kubwa na kuondokana na umaskini.

Alisisitiza kwamba umaskini utaondokana na kujituma hivyo mlango uko wazi kwa wawekezaji na wachimbaji wa madini ya dhahabu kwa sababu tayari kuna soko kuu na masoko mengine madogo ndani ya wilaya hiyo.

"Kiasi cha fedha zaidi ya Shilingi bilioni moja kimekusanywa kutoka kwenye sekta ya madini ya dhahabu wilayani Chunya ambazo zinatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile ujenzi wa vituo vya afya, barabara na shule," alisema Mahundi.

# Auawa kwa kucharangwa mapanga

Na Grace Mwakalinga, MBARALI

MKAZI wa Kijiji cha Mpakani, Ally Mazinge (66), Kata ya Ubaruku katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, ameuawa kwa kukatwa na vitu vyenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili wake na kumsababishia umauti.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema Mazinge aliuawa Juni 26, mwaka huu majira ya saa saba usiku akiwa nyumbani kwake amelala.

Alisema tukio la kuuawa lilifanyika baada ya mke wa marehemu, Chiku Mahamoud, kutoka nje kujisaidia mita saba kutoa chumba alichokuwa amelala marehemu ndipo watu wasiojulikana waliingia na kuanza kumkata kata kwa vitu vyenye ncha kali na kumsababishia umauti.

Alisema kwa mujibu wa uchunguzi wa awali uliofanywa na Jeshi la Polisi, kulikuwa na mgogoro wa kifamilia baina ya marehemu, mke na watoto wakigombea kuuza eneo la nyumba wanayoishi.

Kutokana na tukio hilo watoto wanne wa marehemu na mke wamekamatwa na kupelekwa mahabusu ya Rujewa kwa ajili ya uchunguzi.

"Mke na mtoto wa marehemu kulikuwa na mzozo wa kutaka kugombea eneo la mzee sasa mazingira ya kifo yanaonyesha moja kwa moja kwamba walihusika na tukio hilo, hivyo watu wanne tunawashikilia kwa ajili ya mahojiano zaidi," alisema Matei.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mbuyuni, Francis Mayemba, alisema alipata taarifa za kifo hicho usiku Juni 27 kutoka kwa moja ya wananchi wake wakieleza juu ya kifo hicho.

Alisema baada ya kufika eneo la tukio aliona mwili wa marehemu ukiwa unavuja damu baada ya kucharangwa mapanga mwilini mwake na kutoa taarifa kituo cha polisi na walipofika waliuchukua mwili ili kuufanyia uchunguzi.

Miongoni mwa watoto akiwamo Sada Ally (20) na Ramla Idd (33), walisema walipigiwa simu na mama yao akiwaeleza kutokea kwa tukio hilo ambalo lilifanywa na watu wasiojulikana baada ya kutoka uani kujisaidia.





# Wamiliki wa shule waonywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imewaagiza wamiliki wa shule binafsi wakiwamo walimu wakuu kutotoza ada ya masomo kwa wazazi kuanzia Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Agizo hilo linatokana na serikali kufunga shule zote kwa sababu ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona.

Hatua hiyo ya wizara imetolewa baada ya kubainika kuwa baadhi ya wamiliki wa shule hizo wamekuwa wakiwataka wazazi wa wanafunzi kulipa ada kwa kipindi ambacho wanafunzi hawakuwa shuleni jambo ambalo ni kinyume cha maagizo ya serikali.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Waziri wa Wizara hiyo, Riziki Pembe Juma, alisema serikali iliamua kuzuia mikusanyiko ya watu na kusababisha masomo na shughuli zingine muhimu za kiuchumi na kijamii kusimamishwa.

Pembe alisema wamiliki na walimu wakuu wote wa shule hawatakiwi kuwafukuza wanafunzi kwa kutolipa ada kwa kipindi serikali ilipofunga shule hizo.

Alisema wazazi hawatoruhusika kulipia ada ya miezi iliyopita na badala yake walipe ada hizo kuanzia mwezi huu kwa mujibu wa sheria.

Waziri alisema kumekuwa na mvutano baina ya wazazi na wamiliki wa shule binafsi juu ya kuwalipia ada wanafunzi kwa kipindi ambacho shule zilifungwa.

Alisema ni wajibu kwa wamiliki wa shule hizo kufuata taratibu zote zilizowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara hiyo na kuhakikisha wanatimiza vigezo vilivyowekwa ili kutimiza malengo husika.

Kutokana na hali hiyo, aliwatahadharisha wamiliki wote wa shule hizo kufuata agizo la serikali na watakaokaidi utekelezaji huo, wizara itachukua hatua za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani na kuzifungia shule zao.

"Hatuwezi kuwafumbia macho watakaopinga agizo hili na mtu yoyote atakayebainika kwenda kinyume, sheria itachukua hatua dhidi yake," alisema.

# Ajinadi urais kwa turufu ya wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ADA TADEA, Juma Ali Khatib, amechukua fomu ya kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar kupitia chama hicho.

**Serikali yangu itahakikisha inawalea watoto wote katika mazingira mazuri hasa wale wanaotelekezwa.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuchukua fomu hiyo, Khatib alisema endapo atapitishwa na chama chake na kupata ridhaa ya Wazanzibari kuwa Rais, atahakikisha anaimarisha maisha ya wanawake.

Alisema kila mwanamke atakayejifungua atahakikisha anapatiwa posho maalum ya muda wa miaka miwili ili wanawake wawe na maisha mazuri na kuwalea watoto katika hali nzuri.

Khatib alisema wanawake ni watu muhimu na wengi wanapata usumbufu mkubwa katika kuwalea watoto kwa sababu ya kutelekezwa na baadhi ya wanaume, hivyo watoto kukosa huduma muhimu.

"Serikali yangu itahakikisha inawalea watoto wote katika mazingira mazuri hasa wale wale wanaotelekezwa," alisema.

Sambamba na hilo, alisema atahakikisha anatekeleza miradi yote iliyoanzishwa na Rais Dk. Ali Mohamed Shein, anayemaliza muda wake, ambayo bado haijamalizika. Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni Bandari ya Mpiga Duri, bandari ya mafuta na gesi na kiwanda cha mwani.

"Nitahakikisha miradi hiyo mikubwa naimaliza ili wananchi wapate maendeleo," alisema Khatib ambaye pia ni Waziri Asiye na Wizara Maalum katika Serikali ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa Khatib, Dk. Shein amefanya mambo mengi ya maendeleo, hivyo atafuata nyayo zake hasa katika kudumisha amani na usalama wa nchi.

Alisema serikali imeshaanza kujenga misingi imara ya mikakati ya uchumi, hivyo atahakikisha anakuza na kuendeleza uchumi huo kwa maslahi ya taifa.

Pia alisema atahakikisha anadumisha Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao uliasisiwa na Abeid Amani Karume na Mwalimu Julius Nyerere.

Licha ya kwamba anatokea chama cha upinzani, alisema maendeleo hayachagui chama, hivyo atahakikisha anawaletea wananchi maendeleo bila kujali itikadi zao.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Rashid Mchenga, alimkabidhi fomu mgombea huyo na kumtaka azirejeshe kabla ya kufungwa kwa pazia la kuchukua na kurejesha fomu Julai 7, mwaka huu.




Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ADA TADEA, Juma Ali Khatib (kushoto), akichukua fomu za kugombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hicho, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Samia ataka umoja kwa ushindi CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Makamu wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amewataka Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Kusini Unguja kuendelea kuwa wamoja na kushikamana katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Samia aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wajumbe hao katika kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mikutano wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kilichoko Tunguu, mjini hapa.

Alisema ushindi wa CCM utatokana na ushirikiano baina ya viongozi na wanachama wote.

Samia alisema licha ya mkoa huo kuwa ngome ya CCM, bado wanatakiwa kulinda heshima hiyo kwa kujipanga vizuri kuhakikisha chama kinashinda.

"Nakuombeni tufanye kazi kwa mashirikiano (ushirikiano) makubwa (mkubwa) kwani ushindi wa chama chetu hautapatikana kwa maneno bali kwa juhudi za kila mmoja wetu," alisema Samia.

Pia aliwasihi wajumbe hao kufuata miongozo na kanuni za chama wakati wa kufanya uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi katika mkoa huo, huku akikemea rushwa na makundi kwa kuwa vitendo hivyo vinaweza kusababisha kupatikana viongozi wasio na sifa.

Katika hatua nyingine, Samia alitoa pole kwa wananchi wa mkoa huo kwa kukumbwa na majanga mbalimbali yakiwamo ugonjwa wa corona na mafuriko.

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kutunza mazingira ili kuepuka majanga mbalimbali yakiwamo mafuriko.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, Ramadhan Abdallah Ali, alimpongeza Samia kwa utendaji wake na kuwa karibu na mkoa huo kwa kutoa nasaha za kujenga chama.

Naye Katibu wa CCM wa Mkoa huo, Suleiman Mzee Suleiman, akisoma taarifa ya utekelezaji ya chama kuanzia Januari hadi Machi 30, mwaka huu, alisema wamejipanga vizuri na watahakikisha wanashinda majimbo yote yaliyomo katika mkoa huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NATAFUTA KAZI YA UDEREVA NA SALES,** MIMI IRENE J. BWIRE MWENYE UMRI WA MIAKA 28 NATAFUTA KAZI YA UDEREVA NA SALES. UZOEFU WANGU NI MIAKA 8 SASA. KWA MAWASILIANO NIPIGIE KWA SIMU NAMBA 0689 617313.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### 0FISI YA WASIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MZEE SHABANI IBRAHIM

Ofisi ya wasimamizi wa mirathi ya marehemu Mzee Shabani Ibrahim,(Masoud Mgassa, Marium Ibrahim Karumba na Abbas Ibrahim Karumba) inapenda kutoa tangazo kwamba inategemea kufanya kikao cha wana familia tarehe 11 mwezi wa saba (7) mwaka 2020, nyumbani kwa marehemu kirumba mwanza. Hii kutokana na amri ya mahakama ya mwanzo musoma mjini iliyotaka kikao kifanyike.

Agenda za kikao.

1. kutambua mali za marehemu
2. kutambua madeni na wadai wa marehemu
3. mrejesho wa usimamizi wa mirathi.
4. mengineyo

Tangazo hili limetolewa na

1.Mariam Ibrahim Karumba

..........................................

2.Abbas Ibrahim karumba

..........................................

Mawasiliano :0652 416525/0718197444.

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAZIA MOHAMED FAZAL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 301 DMV TOYOTA DYANA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi:
**TAN/RB/410404/2020.**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JEROME JACKSON MHOGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya FEKON yenye namba za usajili MC 695 AYL, Chassis No.IDAPAJOBLEGB11327, Engine No.157FMI-215F11327. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOD/KON/RB/405831/2020.

### KUPOTEA KWA CHETI



Elizabeth Thomas Mero anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari Kidia chenye Index No S.04575/011 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 1990

Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa polisi: KRT/RB/1407/2020

### KUPOTEA KWA LEAVING CERTIFICATE



DIANA FESTO MGOMAPAYO anatangaza kupotelewa na LEAVING CERTIFICATE Kilichotolewa na AMANI GIRLS mwaka 2019 pamoja na form two result slip. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
taarifa ya polisi:
DOD/DOD/RB/495820/2020.

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi 62/2020**

Ombi la ALFRED E. KIMONGE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu REGISLA CHARLES KIMONGE

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 01/7/2020.

### JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**
**PONGWE - TANGA**

Usimamizi wa Mirathi Na. 14/2020
Ombi la ABDALLAH OMARI HANEIN kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu OMARI ALLY HANEIN
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 01/07/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE


*Kwa Habari Motomoto*
*usikose Gazeti lako la*
*Nipashe kila siku*
*Tupigie*
*0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# 50 wauawa maandamano yakishika kasi

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

WATU wapatao 50 wameuawa kwenye maandamano yanayofanyika katika mji ya Oromiya nchini Ethiopia baada ya kuuawa mwanamuziki maarufu nchini humo.

Watu hao wameuawa wakati walipokuwa wanashiriki kwenye maandamano katika mji huo ambayo yalianza baada ya kuuawa mwanamuziki maarufu nchini humo, Haacaaluu Hundeessaa.

Msemaji wa Jiji hilo, Getachew Balcha, alisema kuwa watu waliokufa ni waandamanaji na maofisa usalama na kusema kuwa baadhi ya sehemu za biashara zimechomwa moto.

**Watu waliokufa ni waandamanaji na maofisa usalama na kusema kuwa baadhi ya sehemu za biashara zimechomwa moto.**

Wakati huo huo, serikali ya Ethiopia imethibitisha kwamba kiongozi wa upinzani nchini humo, Jawar Mohammed, amekamatwa.

Mohammed ambaye hapo awali alikuwa mmiliki wa vyombo vya habari na aliyejiunga hivi karibuni na chama cha Oromo Federalist Congress, alikamatwa juzi katika mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa pamoja na watu wengine 34.

Mkuu wa Jeshi laPolisi nchini Ethiopia, Endeshaw Tassew, alisema kwamba Mohammed alikamatwa baada ya kutokea purukushani na polisi kuhusiana na mwili wa mwanamuziki huyo maarufu aliyepigwa risasi siku ya Jumatatu usiku na tukio hilo likasababisha maandamano makubwa nchini humo.

Mkuu huyo wa polisi ameeleza kwamba kiongozi huyo na wenzake waliingilia kati wakati mwili wa mwanamuziki huyo ulipokuwa unasafirishwa kwa ajili ya mazishi kwenye mji wake wa uzawa wa Ambo.

Alisema wapinzani walitaka kuuchukua mwili huo na kuurudisha mjini Addis Ababa ndipo purukushani ilipotokea. Polisi mmoja wa kikosi maalumu kutoka Jiji la Oromo aliuawa.

Kwa mujibu wa taarifa ya polisi, watu hao waliokamatwa pia walikuwa na bunduki aina ya Kalashnikov, bastola tano na radio za mawasiliano.

Haacaaluu Hundeessaa mwanamuziki kutoka jamii ya Oromo alijulikana kwa nyimbo zake zinazotumiwa sana kwenye maandamano.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, katika ujumbe wake wa Twitter jana alitoa rambirambi na kuahidi kwamba uchunguzi wa kina utafanyika huku akiwataka wananchi kuwa watulivu.

Kwingineko kamati ya kuwalinda wanahabari CPJ imelaani kufungwa kwa mtandao wa intaneti mjini Addis Ababa pamoja na kuvamiwa vyombo vya habari vya Oromia. **DW**

## Mwandishi habari ahukumiwa kifo

**TEHRAN,** Iran

MAHAKAMA nchini Iran imemhukumu kifo mwandishi wa habari ambaye alichapisha andiko kwenye mitandao ya kijamii ambalo lilisaidia kuhamasisha maandamano ya nchi nzima dhidi ya hali ngumu ya kiuchumi mwaka 2017.

Mwandishi huyo, Ruhollah Zam, alikuwa amerejea Iran katika mazingira yasiyofahamika na kisha akawekwa kizuizini.

Msemaji wa mahakama, Gholamhossein Esmaili, ametangaza hukumu hiyo jana.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mwandishi huyo alikuwa akiendesha tovuti iitwayo AmadNews, ambayo ilituma picha za video na taarifa zilizokuwa zikiwakosoa vikali maofisa wa Iran.

Wakati huo alikuwa akiishi na kufanya kazi zake mjini Paris, Ufaransa, kabla ya kushawishiwa kurejea Iran, ambako alikamatwa Oktoba mwaka jana.

Zam alijitokeza baadaye kwenye Televisheni ya umma, akikiri na kuomba radhi kwa makosa aliyofanya. **DW**

## Maduro amtimua balozi wa EU

**CARACA,** Venezuera

RAIS wa Venezuela, Nicolas Maduro, ametoa muda wa saa 72 kwa balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) awe ameondoka katika ardhi ya Venezula kabla hatua kali hazijachukuliwa, vyombo vya habari nchini humo vimebaini.

Hatua hiyo inakuja baada ya Umoja wa Ulaya kuchukulia vikwazo kundi la wawakilishi wa Venezuela kwa hatua zao dhidi ya Baraza la Congress ambapo upinzani una viti vingi.

Wakati huo huo, Umoja wa Ulaya (EU) umelaani hatu hiyo ya kufukuzwa kwa balozi wake nchini Venezuela.

Mkuu wa sera ya kigeni wa EU, Josep Borrell, amelaani hatua hiyo ya Rais wa Venezuela na kutangaza hatua za "kukabiliana" na uamuzi huo. **RFI**



Wananchi wa Ethiopia wakiwa katika maandamano baada ya kuuawa kwa mwanamziki mwanaharakati, Haacaaluu Hundeessaa. **PICHA: REUTERS**

# Mataifa 14 yaruhusiwa kuingia Ulaya

**WASHINGTON,** Marekani

UMOJA wa Ulaya (EU), umetaja majina ya nchi 14 ambazo wananchi wake wanadaiwa kuwa salama kuruhusiwa kuingia katika nchi zake kuanzia Julai mosi, mwaka huu licha ya mlipuko wa ugonjwa wa corona kuwapo.

Lakini katika jambo la kushangaza nchi za Marekani, Brazil na China hazipo katika orodha hiyo.

Mataifa yaliyotajwa ni pamoja na Australia, Canada, Japan, Morocco na South Korea.

Muungano wa Ulaya upo tayari kuiongeza China katika orodha endapo serikali ya nchi hiyo itatoa ruhusa sawa kwa wasafiri wa EU.

Makatazo katika mipaka ya EU imeondolewa kwa wasafiri ambao ni raia wanaotoka katika umoja huo.

Sheria zilizowekwa dhidi ya wasafiri wa Uingereza ziko tofauti na makubaliano ya Brexit.

Wananchi wa Uingereza wanachukuliwa sawa na raia wa Muungano wa Ulaya mpaka mwisho wa kipindi cha mpito cha Desemba, 31.

Katika orodha ya sasa, maeneo salama ambayo yanaweza kuongezwa ni nchi za Algeria, Australia, Canada, Georgia, Japan, Montenegro, Morocco, New Zealand, Rwanda, Serbia, South Korea, Thailand, Tunisia na Uruguay.

Kwa sasa Uingereza inafanya majadiliano na mataifa kadhaa ambayo ni wanachama wa EU kuona namna ambavyo virusi vya corona vinaweza kutozuia mapumziko ya wakati wa msimu wa watalii unaowaajiri mamilioni ya watu.

Mataifa mengi ya EU - yapata asilimia 55 ya mataifa ya Umoja wa Mataifa (UN), ambayo ni sawa na asilimia 65 ya idadi ya watu wa EU ambao wako kwenye orodha.

Kuna mgawanyiko kati yao kama vile Hispania ambayo inataka kukuza utalii lakini inataka kujionyesha salama licha ya ugonjwa wa corona kuathiri nchi hiyo kwa ukubwa.

Nchi nyingine ni Ugiriki na Ureno ambazo zote zinategemea utalii lakini wanaogopa virusi. **BBC**

# SOLSKJAER ASIFIA KIWANGO CHA UNITED




**MANCHESTER,** England

MPANGO wa Manchester United kuamua kucheza kwa kujilinda kwa umoja ndio mafanikio ya timu hiyo kwa siku za hivi karibuni, kwa mujibu wa kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Mashetani wekundu hao wamekuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu kurudi tena kwa ligi hiyo baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, wakipata pointi tatu kwenye mechi zao tatu za Ligi Kuu na kutinga hatua ya nusu fainali ya FA baada ya kuifunga Norwich City.

Kikosi hicho Jumanne kilipata ushindi wa mabao 3-0, shukrani kwa mabao mawili ya Bruno Fernandes na moja ya Mason Greenwood dhidi ya Brighton and Hove Albion pale kwenye dimba la Amex na kuirudisha kwenye nafasi ya tano katika msimamo, mbili tofauti na Chelsea. Kwa matokeo hayo maana yake ni kwamba United imeruhusu nyavu zake kutikiswa mara mbili tu katika mechi nane zilizopita za Ligi Kuu England, huku Solskjaer akielezea sababu ni kucheza kwa umoja na kujilinda.

"Unaweza kuona ubora wa timu na vipaji vya wachezaji wangu na jinsi wanavyocheza kwa umoja kwa sasa," alisema.

"Tumejiweka kwenye nafasi nzuri na kikosi kipo kwenye wakati mzuri na kwa namna ya pekee, tunacheza kwa umoja na mafanikio nayaona."

# Mkhitaryan apewa mkataba mpya Roma

**ROME,** Italia

HENRIKH Mkhitaryan ataendelea kubakia kwa mkopo pale AS Roma kwa msimu mmoja zaidi, huku miamba hao wa Serie A pia wakibainisha kuwa atakaa nchini Italia kwa mwaka mmoja zaidi.

Mkhitaryan amecheza mechi 19 katika mashindano yote msimu huu tangu ajiunge nao akitokea Arsenal Septemba, mwaka jana na amerudi dimbani hivi karibuni akitokea majeruhi.

Roma sasa wataendelea kuwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Armenia ambaye ameonyesha kiwango cha kuvutia kwa miamba hao.

"Nina furaha kubwa," alisema Mkhitaryan – ambaye alianza katika mechi mbili zilizopita.

"Nina furaha kuongeza muda hapa, kwa sababu bado nina vitu ambavyo sijafanikiwa kuvifanya na nataka kuvifanya.

"Naangalia kutaka kuendelea kucheza zaidi."

Mkhitaryan alihamia kwa Washika Bunduki hao kutoka Manchester United Januari mwaka 2018 katika uhamisho uliomhusisha Alexis Sanchez kwenda upande mwingine.






# *Ronaldo, Dybala wamejifunza kucheza pamoja – Sarri*

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo na Paulo Dybala wamejifunza kufanya kazi pamoja baada ya kufunga mabao, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Juventus, Maurizio Sarri.

Ronaldo na Dybala wote walifunga mabao wakati Juve ikiendelea kubakia kileleni mwa msimamo kwa pointi nne zaidi katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Genoa.

Kumekuwa na shaka kwamba, Ronaldo na Dybala hawafiti kucheza pamoja pale Juve katika kikosi cha kwanza, lakini wawili hao walianza wote kwenye mchezo huo wa Jumanne.

Sarri aliwasifia akiiambia Sky Sport Italia: "Vitu fulani vimebadilika kwa wakati huu, lakini wamejifunza kucheza kwa pamoja.

"Wamekubali kwamba, wanaweza kucheza pamoja na sasa wameweza kufanya hivyo. Kuna kitu ambacho nilikiona kwenye mazoezi na sasa wanafanya vizuri."

Dybala alianza kwa kufunga bao dakika ya 50 kabla ya Ronaldo kufanya matokeo kuwa 2-0 dakika sita baadaye.

Bao la tatu la Juve lilifungwa na Douglas Costa, kabla ya Andrea Pinamonti kuwafungia Genoa bao la kufutia machozi dakika ya 76.

## HABARI MICHEZO

# Lampard akanusha kumhitaji Gomes

**LONDON,** England

FRANK Lampard amekataa kuwa Chelsea ina mpango wa kumsajili winga wa Manchester United, Angel Gomes.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 19 mkataba wake umemalizika pale Old Trafford na Ole Gunnar Solskjaer alisema Jumatatu kwamba, anatarajia Gomes ataondoka klabuni hapo baada ya kutomwongezea mkataba.


Magazeti ya Uingereza yalidai Gomes amewekewa mkataba mezani pale Chelsea, lakini Lampard aliwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana Jumatano dhidi ya West Ham, kwamba jambo hilo halijui.

"Naweza kusema kwamba, sijui chochote kuhusu huyo mchezaji mnayemtaja. Ni hivyo tu," alisema Lampard.

Lampard aliongeza kusema kwamba, yeye binafsi hajapata taarifa juu ya mpango wa kumsajili mchezaji huyo.

Chelsea wanatajwa kuwa wamekamilisha usajili wa Hakim Ziyech na Timo Werner kutoka Ajax na RB Leipzig.

Jana Jumatano nyota hao walikuwa wachezaji rasmi wa Chelsea baada ya kukamilisha usajili wao.






# HATIMAYE SANE ASAJILIWA BAYERN

**MANCHESTER,** England

LEROY Sane amekamilisha usajili wa kutoka Manchester City kwenda Bayern Munich, kwa mujibu wa Sky Sport.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani atawagharimu Bayern ada ya awali ya euro milioni 49, ambapo inatarajia kupanda hadi euro milioni 60 na jana Jumatano alitarajiwa kukamilisha usajili huo.

Sane alijiunga na City kutoka Schalke mwaka 2016 katika dili ambalo liliripotiwa kuwa pauni milioni 37 na akawa na kiwango cha kuvutia katika msimu wake wa kwanza.

Alishinda mchezaji bora kijana msimu wa 2017/18 wakati kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kikitwaa taji la Ligi Kuu England.

Sane aliisaidia City kutwaa tena taji mwaka uliofuata wakati akifunga mabao 16 kwenye mashindano yote, ingawa kwa muda mrefu alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu hiyo ya Ujerumani.

Bayern waliripotiwa kuwania kutaka kumrudisha winga huyo kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, mwaka jana, hata hivyo walishindwa kufikia bei iliyotakiwa.

Sane aliumia goti kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii na amecheza mara moja tu tangu kurudi kwa ligi hiyo tangu mapema Juni.

# Arteta: Natarajia Ozil amechukia

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anatarajia Mesut Ozil kuchukizwa na kutopata nafasi ya kucheza mara kwa mara pale Arsenal, lakini amesisitiza tena bado yupo nyuma ya mchezaji huyo.

Ozil hajacheza mchezo wowote tangu kurudi kwa msimu huu, licha ya kuwa kwenye mechi zote za Arsenal za Ligi Kuu England chini ya Arteta kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya Arsenal kuivaa Norwich City jana, Arteta alisisitiza umuhimu wa mchezaji huyo wa Ujerumani kwenye kikosi chake.

Arteta amekubali kwamba Ozil bado hajawa kwenye kiwango cha kumfanya arudi dimbani, lakini akasisitiza mshindi huyo wa Kombe la Dunia bado ni mchezaji muhimu kwa Washika Bunduki hao.

"Natarajia mchezaji ambaye hapati nafasi ya kucheza kuumizwa na hali hiyo," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Naamini hana furaha kwa sababu hapati nafasi ya kucheza, na naamini anaelewa hivyo, na kwamba atajituma ili arudi uwanjani.

"Nataka wachezaji wote kucheza kwenye kiwango chao cha ubora na wanatakiwa kucheza kwa uwezo wao wote."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AWEKA REKODI MPYA

## Ni baada ya kufikisha mabao 700 tangu alipoanza kucheza kandanda, huku Barcelona...

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI Lionel Messi amefikisha mabao 700 tangu alipoanza kucheza soka baada ya kufunga penalti aina ya Panenka wakati Barcelona ikitoka sare kwenye mechi ya La Liga na Atletico Madrid hapo Jumanne usiku.

**Mfungaji bora huyo wa vigogo hao wa Hispania alifikisha idadi hiyo ya mabao kwa kuifungia klabu pamoja na nchi yake kwa kumpeleka 'boya' golikipa Jan Oblak.**

Goli hilo lililofunga liliifanya Barcelona kuongoza kwa mabao 2-1, lakini baadaye Atletico ilisawazisha na mechi hiyo kumalizika kwa sare ya magoli 2-2.

Barca imeendelea kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa La Liga, ikiwa pointi moja nyuma ya Real Madrid, ambayo ina mechi moja mkononi.

Penalti hiyo iliyofungwa na Messi ni bao lake la 630 kwa klabu hiyo ambayo ameichezea michezo 724.

Messi aliipeleka katika uongozi Barcelona kwa mpira huo maarufu kwa jina la Panenka, lakini Saul Niguez aliisawazishia timu yake na kuifanya Barca kupoteza pointi ambazo zinawaathiri kwenye mbio zake za kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

Mshambuliaji huyo amefikisha mabao 700, ikiwa ni miezi 14 imepita tangu alipofikisha mabao 600 kwa Barcelona, na kujiunga katika orodha ya nyota wengine waliowahi kutamba kwa kupachika mabao mengi.

Kwa mujibu wa takwimu za Taasisi ya Rec.Sport.Soccer, Messi ni mmoja kati wa wachezaji saba ambao wamefanikiwa kufikisha mabao 700 tangu aanze kusakata kandanda.

Nyota mwenye asili ya Jamhuri ya Czech na Austria, Josef Bican anaongoza kwa kupachika mabao 805 akifuatiwa na mkongwe kutoka Brazil, Romario aliyefunga magoli 772, huku Pele akishika nafasi ya tatu kwa kufunga mabao 767.

Mshambuliaji wa Hungary, Ferenc Puskas yeye alifunga mabao 746 huku straika wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Gerd Muller alifunga mabao 735.

Mpinzani wa karibu wa Messi katika ufungaji mabao, Cristiano Ronaldo, anashika nafasi ya sita baada ya kufikisha magoli 700 katika mchezo kati ya timu yake ya Taifa ya Ureno ilipokutana na Ukraine kwenye mechi za kusaka tiketi ya kushiriki Kombe la Euro 2020, iliyochezwa Oktoba mwaka jana.

Ronaldo tayari ameshafunga mabao mengine zaidi 26 baada ya hapo.

## ZISIKUPITE

### UNITED, DORTMUND ZAVUTANA

MANCHESTER United imesema haitalipa zaidi ya pauni milioni 50 ili kumsajili winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho. Hata hivyo, vigogo hao wa Bundesliga wanataka kulipwa zaidi ya pauni milioni 100 ili kumwachia nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL KUMTOA GUENDOUZI

ARSENAL imemweka kiungo wake Mfaransa, Matteo Guendouzi, ambaye ana umri wa miaka 21, kama sehemu ya mchakato wa kunasa wachezaji wapya wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa. ***(Mail)***

### HOJBJERG KUTUA SPURS

TOTTENHAM inaamini itafanikiwa kunasa saini ya kiungo wa Southampton na Timu ya Taifa ya Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg (24), ifikapo majira ya joto lakini italazimika kuuza wachezaji wake wengine. ***(Telegraph - subscription required)***

### CITY, CHELSEA VITANI

MANCHESTER City inajiandaa kumsajili beki wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Nathan Ake. Hata hivyo watakutana na ushindani kutoka kwa Chelsea, ambayo imeonyesha nia ya kumrejesha klabuni hapo beki huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic - subscription required)***

### JIMENEZ MAMBO MAZURI

STRAIKA wa Wolves ambaye ni nyota wa kimataifa wa Mexico, Raul Jimenez (29), amesema anafahamu tetesi zinazomhusu kuhusiana na uhamisho na anafurahi kuona klabu mbalimbali zinamzungumzia. ***(Telemundo via Mail)***

### JURADO KUTUA UNITED

BEKI wa kulia wa Barcelona, Marc Jurado (16), ameondoka Katalunga na Mhispania huyo anajiandaa kujiunga na Manchester United katika majira ya joto. ***(ESPN)***

### TORRES ATAKIWA JUVE

JUVENTUS imeongeza nguvu katika kuwania saini ya nyota wa Valencia, Ferran Torres (20). Winga huyo wa Hispania pia anahusishwa na mipango ya kujiunga na Manchester United pamoja na Borussia Dortmund. ***(Onda Cero via Mail)***

### BARCA 'KUMFUNGA' PJANIC

BARCELONA imeweka dau la pauni milioni 365 katika mkataba wa Miralem Pjanic endapo atataka kuondoka klabuni kwao. Kiungo huyo wa Bosnia na Juventus ambaye ana umri wa miaka 30, anajiandaa kujiunga na vigogo hao wa Hispania ifikapo majira ya joto. ***(Sun)***

### HAKIMI AKARIBIA INTER

BEKI wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Morocco, Achraf Hakimi (21), anatoa kipaumbele cha kujiunga na timu ya Italia, Inter Milan ambayo imeweka dau la pauni milioni 36. ***(Mail)***

### MKHITARYAN KUBAKI ARSENAL

ROMA imethibitisha mkataba wa mkopo wa Henrikh Mkhitaryan ndani ya kikosi cha Arsenal utaendelea hadi mwisho wa msimu. Kiungo huyo raia wa Armenia ambaye ana umri wa miaka 31, alijiunga na klabu hiyo ya Serie Septemba, mwaka jana. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

## Jang'ombe yalilia mashabiki Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KLABU ya Jang'ombe Boys imeiomba serikali kuruhusu mashabiki kuingia viwanjani katika mechi za Ligi Kuu Zanzibar ili timu zinazoshiriki ligi hiyo kupata fedha za kusaidia kuhudumia wachezaji na gharama nyingine za utawala.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliruhusu Ligi Kuu Zanzibar kurejea, lakini ilitoa uamuzi wa kuchezwa bila mashabiki kwa ajili ya kuendelea kujikinga na virusi vya corona.

Rais wa Jang'ombe Boys, Ali Othman "Kibichwa" alisema wanaishukuru serikali kwa msaada wa fedha walioutoa kwa timu zote ili kuendelea na ligi hiyo, lakini ni vema pia wakaruhusu mashabiki kuingia uwanjani ili kuongeza mapato. Kibichwa alisema timu yao hivi sasa ipo katika hali ngumu kutokana na janga la corona na wanaamini fedha zitakazopatikana kutoka kwenye viingilio, itasaidia kupungua makali ya kuihudumia timu.

"Vilabu vya kiraia vinahitaji pesa kwa ajili ya kumalizia ligi, na hii inatokana na ligi yenyewe kutokuwa na mdhamini, hata timu pia hazina wadhamini binafsi hali inayopelekea kushindwa kumudu huduma mbalimbali za uendeshaji, hususani katika kipindi hiki cha kumalizia msimu," Kibichwa alieleza.

Hata hivyo aliliomba Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kuendelea na jitihada zake kuzisaidia timu katika kipindi hiki cha lala salama ili msimu umalizike kama ilivyokusudiwa.

## 'Date my Family' kuonekana rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kufundisha kuelekea katika maisha mapya, kipindi cha mahusiano kijulikanacho kwa jina la 'Date my family' kitaanza kuonyeshwa kwenye Chaneli ya Maisha Magic Bongo iliyoko DSTV kuanzia leo na kitaonekana katika vifurushi vyote, imefahamika.

Kipindi hiki cha aina yake cha mahusiano humuonyesha kijana katika hatua zake za kuchumbia lakini tofauti na ilivyozoeleka, hapa kijana atakuwa anawasiliana na familia za wachumba watarajiwa na hatimaye kufanya uamuzi wa mchumba kabla hata hawajaonana.

"Date My Familiy ni kipindi kinachohusu mahusiano hivyo kinawaunganisha watu wenye tabia zinazofanana, ambapo kijana anayetaka mchumba atakutana na familia tatu tofauti zenye wachumba watarajiwa na baada ya mazungumzo na familia hizo mchumbiaji ataamua kumposa mchumba mmoja," alisema Ronald Shelukindo, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania.

Kulingana na mazungumzo ya kina baina ya mchumbiaji mwenyewe na familia ya mchumba, kijana atapata fursa ya kumfahamu vizuri mchumba wake bila kumuona.

"Baada ya kukutana na familia hizo, mabachela au warembo hao watachagua familia waipendayo na hatimaye kwenda kukutana na mchumba husika," alisema Shelukindo.

# MAXIME AKATAA KUJADILI 'MAUZAUZA' YA WAAMUZI

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema anawaachia Watanzania walioshuhudia mechi yao dhidi ya Yanga kutoa uamuzi wa mwisho juu ya waaamuzi waliochezesha mchezo huo wa hatua ya robo fainali.

**Kagera Sugar iliondolewa katika michuano hiyo juzi baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1, kutoka kwa Yanga.**

Maxime alisema hawezi kuzungumza lolote kuhusiana na kiwango kilichoonyeshwa na waamuzi katika mechi hiyo ambayo wachezaji wake walionyesha kandanda la kiwango cha juu.

"Sina mengi ya kuongea, wachezaji wangu wamecheza vizuri, ila suala la mwamuzi (Shomari Lawi), hilo nawaachia Watanzania watakuwa waamuzi wa mwisho," alisema nahodha huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Naye kiungo wa Kagera Sugar, Awesu Awesu alisema hajui sababu ya yeye kuonyeshwa kadi ya pili ya njano iliyobadilika na kuwa nyekundu katika mchezo huo.

"Sikuongea lolote wakati ninaonyeshwa kadi ya kwanza, tena nilishangaa namna nilivyopewa nikasema sawa, kadi ya pili nilikuwa nimechezewa faulo nikawa namtoa, Abdallah Seseme maana alikuwa na jazba, nashangaa nakutana na kadi nyingine, sijui ilikuaje, sijaongea jambo lolote na wala sijatukana, aulizwe hata refa mwenyewe," alisema Awesu.

Kiungo huyo alisema matokeo waliyopata hayajamshangaza kwa sababu walicheza na timu kubwa na kongwe ambazo wasimamizi huingia na maagizo.

"Tunapocheza na hizi timu tunajua kila mmoja anaingia na matokeo yake, hivyo kufungwa sijashangaa ni jambo la kawaida, sababu Yanga wasingekubali kufungwa mara mbili, hivyo wangetumia njia yoyote," Awesu alisema.

Aliongeza kadi hiyo inamuumiza sababu imeigharimu timu yake na bado wana mechi ngumu za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaelekea ukingoni.




Mwandaaji wa filamu nchini, Aziz Mohamed akiwa na baadhi ya wasanii na wadau wa sanaa wakati wa uzinduzi wa kipindi kipya cha mahusiano cha 'Date my Family' ambacho kitaanza kuonyeshwa kuanzia leo kwenye king'amuzi cha chaneli ya Maisha Magic Bongo ya DSTV. **NA MPIGAPICHA WETU**

# JKT Tanzania yaikimbiza Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Mohammed Abdallah 'Bares' amesema lengo namba moja la timu yake ni kuhakikisha wanamaliza msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20 wakiwa katika nafasi tano za juu.

Kwa sasa JKT Tanzania yenye pointi 47, ipo katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza mechi 32.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Bares alisema kikosi chake kipo tayari kwa ushindani na anaamini wachezaji wake watapambana kupata matokeo mazuri katika mechi zake zilizobaki.

Bares alisema kuna ushindani mkubwa katika ligi hasa kipindi hiki cha lala salama kwa kila timu kuhitaji pointi ili kujiokoa na janga la kushuka daraja.

"Ushindani ni mkubwa, hilo lipo wazi ila chochote kinaweza kutokea katika ligi, hatujakata tamaa, bado tunapambana ili kuona namna gani tunafika malengo yetu," alisema Bares.

Kocha huyo alisema mikakati yake ni kupata matokeo mazuri katika mechi mbili za ugenini dhidi ya Namungo FC ambayo watacheza kwenye Uwanja wa Majaliwa Julai 4 na 8, mwaka huu watawafuata Ndanda FC kwenye dimba la Nangwanda Sijaona, Mtwara.

"Kikosi changu kipo vizuri hakuna majeruhi, tutamkosa Mwinyi Kazimoto katika mchezo dhidi ya Namungo kwa kutumikia adhabu ya kadi nyekundu, atarejea tena katika kampeni yetu tutakokwenda Mtwara kuivaa Ndanda," alisema Bares.

# Michezo

Alhamisi Julai 2, 2020
Nipashe



Messi aweka rekodi mpya UKURASA 22



Beki wa Yanga, Juma Abdul (kushoto), akijaribu kumtoka mshambuliaji wa Kagera Sugar, Awesu Awesu katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Hatimaye Shiboub arejea kuvaa medali

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ukisema utafurahi kuona wanachukua Kombe la FA, kiungo wake wa kimataifa kutoka Sudan, Sharaf Shiboub, amerejea nchini jana.

Shiboub alikuwa amekwama nchini kwao Sudan kwa sababu ya 'lockdown' iliyosababishwa na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona ambao ulisumbua dunia.

Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema nyota huyo amerejea nchini na ataungana na wenzake kwa ajili ya kumalizia michezo ya ligi iliyobakia na michuano ya Kombe la FA, endapo watasonga mbele.

Rweyemamu alisema ujio wa kiungo huyo, unakamilisha kikosi chao, na wanafurahi kuona nyota huyo atakuwa sehemu ya wachezaji watakaovaa medali siku watakayokabidhiwa kikombe cha ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara. Naye Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck aliliambia gazeti licha ya kutwaa ubingwa wa Bara, timu yake imekabiliwa na ratiba ngumu ambayo wameicheza kwa mikakati.

"Tumetoka kucheza mechi mbili hivi karibuni ambazo zilikuwa ni ngumu kwetu, licha ya kuwa tumeshafanikisha lengo la kutwaa ubingwa, bado tunahitaji kushinda mbele ya Azam FC," alisema kocha huyo kabla ya kushuka dimbani jana.

# Yanga yatamba haishikiki

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

## ●●● Kocha Mbelgiji afunguka wanalihitaji zaidi Kombe la FA, amwondoa Morrison katika mipango yake...

TUNALIHITAJI! KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael amewataka wachezaji wake kuachana na matokeo ya mechi iliyopita, na badala yake kuweka nguvu kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA bila kujali watakutana na nani.

**Yanga ilifanikiwa kusonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwaondoa Kagera Sugar kuwafunga mabao 2-1 katika mchezo wa hatua ya robo fainali uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.**

Kwa ushindi huo, Yanga sasa itakutana na mshindi wa mchezo wa robo fainali nyingine ya mwisho inayowakutanisha Simba dhidi ya mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Azam FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Eymael alisema haikuwa kazi rahisi kusonga mbele, hivyo wanahitaji kuongeza nguvu ili wafanye vizuri katika mchezo wa hatua inayofuata.

Eymael alisema anawapongeza wachezaji wake kwa morali waliyoionyesha kwenye mechi hiyo licha ya kutanguliwa kufungwa bao, na kuwataka waendelea kujituma ili wafikie malengo.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa namna walivyopambana, kwa sasa nataka walekeze mawazo yao kwenye michezo mingine, huu (dhidi ya Kagera Sugar) umepita, FA ndio kombe ambalo tunalipigia mahesabu kwa sasa," alisema Eymael.

Mbelgiji huyo aliongeza jambo kubwa ambalo liko mbele yao ni kuhakikisha wanayakua kombe hilo ili kujihakikishia nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

"Tuna michezo imebaki ya ligi, lakini kwa sasa Kombe la FA ni muhimu zaidi, kwa sababu tayari ligi ni kama imeisha kwa sababu bingwa ameshapatikana, mashabiki waendelee kutusapoti na sisi tutapambana kuhakikisha tunafanya vizuri kwenye FA.

"Nipo tayari kukutana na Azam au Simba ambao ni mabingwa, tutacheza vizuri, nina imani tukikutana utakuwa mchezo mzuri na wenye ushindani mkubwa, tumejipanga kulichukua kombe hilo, ndio malengo na mikakati tuliyonayo," Eymael aliongeza.

Aliweka wazi anatamani zaidi kukutana na Simba katika hatua hiyo inayofuata na anaamini mchezo utakuwa mzuri kwa sababu watani zao hao hucheza mpira mzuri na wakuvutia kila wanaposhuka uwanjani.

Kocha huyo alisema amechukizwa na kitendo cha utovu wa nidhamu ulionyeshwa na kiungo mshambuliaji wake, Bernard Morrison kwa kutoroka kambini.

Alisema hataki kusikia habari za mchezaji huyo pia amemwondoa katika mipango yake kwa sasa kutokana na tabia hiyo aliyoionyesha wakati timu yao ikiwa kwenye 'vita' ya kusaka nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

"Sitamjumuisha katika kikosi changu endapo atarudi, kitendo cha kuondoka bila ruhusa ni utovu wa nidhamu ambao hakuna mtu atakubaliana na tabia hiyo," alisema Eymael.

Alieleza mchezaji anayejitambua hawezi kuondoka kambini wakati timu yake ina mechi ngumu ya kusaka tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa baada ya kushindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

"Hii ni nafasi hatutaki kupoteza, Yanga sio ya mchezaji mmoja, tunapopata ushindi ni wetu sote, kila mmoja tunasimama katika mstari mmoja kufikia malengo yetu," kocha huyo aliongeza.

Mkongomani, David Molinga na Deus Kaseke walifunga mabao kwa upande wa Yanga wakati goli pekee la Kagera Sugar lilipachikwa wavuni na Awesu Awesu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >